

# HADITHI YA UKOMBOZI



# HADITHI YA UKOMBOZI



# HADITHI YA UKOMBOZI

Kimegeuzwa kwa mtindo mpya na Peggy Cummins

**BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH**

Africa Coordinated Curriculum for Bible Study

Y2 - 4Ps

Used with permission of International Publications Services

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

© Copyright, 1987
Baptist Publications House
All rights reserved

## KUHUSU MWANDISHI

Kitabu hiki kimegeuzwa kwa mtindo mpya na Peggy Cummins. Alitumia kitabu cha International Publications Services, *The Story of Redemption.*

Bi Cummins alisomea katika chuo cha Laredo Junior College, Southwest Texas State College and University of Texas, vyote vya huko Amerikani. Yeye na mumewe, Al, ni wamisheni pale Nakuru, Kenya. Wanao watoto wawili wavulana ambao wanaishi Amerikani.

Yeye ni mshiriki wa kanisa la Kibatisti la Nakuru.

## MSALABA NA MAISHA YA KRISTO

1. Mtu anapokuwa Mkristo anatarajia nini?

2. Mkristo anayo mawazo yapi tofauti na mtu asiye Mkristo kuhusu kuwa na mali katika dunia hii?

3. Je, Mkristo anaweza kukubaliana na matakwa ya dunia? Je, Mkristo afanye nini kuhusu haya mambo yafuatayo: kusema uwongo, kudanganya, kupokea rushwa?

4. Nini maana ya kujikana kwa Mkristo? Kwa nini ni muhimu.

5. Paulo alisema, "Kuishi ni kwa ajili ya Kristo na kufa ni faida." Ni rahisi zaidi kuishi kwa Kristo au kufa kwa ajili yake? Orodhesha njia unaweza kuishi kwa Kristo kila siku.

6. Mkristo anawezaje kushiriki msalaba wa Kristo leo?

muhimu katika maisha ya watu wa Mungu. Yesu mwenyewe aliomba kila mara na aliwafundisha wanafunzi wake umuhimu wa kuomba.

Nne, Mkristo anatakiwa ashinde uovu kwa kutenda mema. Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kulipa wema kwa uovu. Jambo hili wakati mwingine sio rahisi, lakini kwa nguvu za Mungu anazotupa, vitu vyote vinawezekana.

Wakristo wanapaswa kufahamu ya kuwa njia ya kushinda uovu ni kutenda mema. Hata hivyo kuna wale ambao hawapo tayari kuupokea upendo wa Mungu. Lakini ni jukumu la Mkristo kujaribu. Ni Roho Mtakatifu peke yake ndiye awezaye kuleta mabadiliko.

Mungu amelipa deni kubwa kwa wokovu wa Mwanadamu. Kama mwanadamu angeweza kununua wokovu wake, basi angeweza kusema uwongo, hata kuua, kudanganya, na hata kuiba ili apate fedha za kulipa kwa ajili hiyo. Fedha haziwezi kununua wokovu. Neema na upendo wa Mungu umekwisha kulipa deni hilo. Watu wengi bado hawajaelewa jambo hili. Wanafikiri ya kuwa kitu cho chote ambacho ni bure hakina thamani. Yesu alilipa gharama hiyo. Ili tuweze kupata uzima wa milele, twapaswa kukubali malipo haya.

Maisha ya Mkristo kila mara yanapaswa yaelekee kwenye msalaba. Msalaba ndio unaomwongoza Mkristo katika utumishi. Unamwongoza pia katika kupata amani na furaha katika Yesu Kristo Bwana wetu. Kutangaza kwa wengine habari njema ni njia moja ya kuishi kwa ajili ya Yesu kila siku.

**Kazi ya Kufanya**

Jadili na rafiki yako Mkristo maswali haya yafuatayo au u andika majibu yake:



## YALIYOMO


| SURA | | UKURASA |
|---|---|---|
| 1. | Uumbaji wa Mungu - Kuanguka kwa Mwanadamu | 7 |
| 2. | Asili ya Dhambi | 12 |
| 3. | Mshahara wa Dhambi | 17 |
| 4. | Ahadi ya Mungu ya Msamaha | 22 |
| 5. | Mungu Alituahidi Masihi | 27 |
| 6. | Mpango wa Mungu na Ukombozi | 32 |
| 7. | Mpango wa Mungu Upo Katika Historia | 37 |
| 8. | Mpango wa Mungu Wahusu Wokovu | 42 |
| 9. | Msalaba Na Ukombozi | 47 |
| 10. | Msalaba na Nafsi ya Kristo | 51 |
| 11. | Msalaba na Tabia ya Mungu | 56 |
| 12. | Msalaba ni Ushinde wa Dhambi | 61 |
| 13. | Msalaba na Maisha ya Kristo | 65 |

juu sana) uwe ndani yetu ili ukae tu. Furaha ya wokovu wetu inatokana na kushirikiana na wengine.

Katika Marko 8:36 swali muhimu sana limeulizwa, Itamfaidi mtu nini kuupata ulimwengu wote?" Hilo ni jambo la muda tu. Hutaweza kwenda na ulimwengu paradiso.

Kila mtu anapaswa kutambua ya kuwa kupata aibu kwa sababu ya kumshuhudia Kristo au kwa sababu ya kulivaa jina lake kutawaletea mateso kabla ya ile siku ya hukumu katika kiti cha Mungu. Kumkataa Yesu leo, baadaye kutakuletea kukataliwa na Mungu siku ya hukumu mbele ya kiti chake.

**Mafunzo Ya Sura Hii Kwangu**

Biblia inatuambia ya kuwa msalaba wa Kristo ni kitu kinachomhusu kila Mkristo. Soma 1 Petro 2:20-25 na 4:12-19. Mkristo anawezaje kuhusiana na msalaba? Nitawezaje kuishi kwa ajili ya Kristo kila siku?

Kwanza kuna kujikana. Marko 8:34 inatusaidia ili tuweze kuelewa ya kuwa jambo hili ni la lazima. Maana yake si kuwa, Mkristo asiwe na vitu vya anasa. Mkristo kuishi maisha ya kujikana maana yake ni kuwa atajitoa yeye mwenyewe kwa kumtumikia Kristo pamoja na watu wengine.

Pili Mkristo anapaswa kuzitangaza habari njema za Yesu, Mkombozi ambaye alikufa kwa ajili ya watu wote mahali pote. Habari hizi lazima zitangazwe na ziwe sehemu ya maisha yetu kila siku.

Kila Mkristo anapaswa kupigana na giza la dhambi kwa kutangaza habari njema za wokovu kwa njia ya imani katika Kristo.

Tatu, Mkristo anapaswa awe mtu wa sala. Katika kuisoma Biblia yako bila shaka umeweza kuona jinsi sala ilivyokuwa

ni mchafu katika utumishi wake. Ili Kristo aweze kufanya kazi katika maisha ya mtu lazima ajiweke tayari na aoshwe kwa damu ya Yesu. Kwa njia hii Mungu anaweza kuingia ndani yake na kumtumia mtu huyu.

**Maelezo**

Hii ni hadithi tu ambayo ilielezwa na mwalimu ila inaweza kutuongoza ili tuweze kuelewa Marko 8:34 vizuri zaidi. Kifungu hiki kinatueleza ya kuwa ni jambo muhimu kwa kila mtu kujitawala yeye mwenyewe. Tamaa zetu sio muhimu katika kutimiza mapenzi ya Mungu. "Kujikana mwenyewe" ni kusema "hapana" kwa tamaa za mwili.

Mungu ni Mungu mwenye haki. Hawezi kuvumilia maisha ambayo yanapingana na kusudi lake. "Kuchukua msalaba wako na kumfuata" ni kusema "Ndiyo" katika kufuata mfano wa maisha ya Yesu yaani kuwapenda na kuwatumikia wengine.

Je, Mkristo anatarajia nini? Katika Marko 8:34-38 Yesu anawaonya wafuasi wake ya kuwa watapata mateso. Aliwaambia ya kuwa haitakuwa rahisi kuwa wanafunzi wake. Ila kuna tumaini kwa yule anayeamini.

Katika Marko 8:35 Yesu anasema ya kuwa mtu atakayethamini maisha yake zaidi kuliko utumishi wa Kristo, mwishowe atapoteza maisha yake. Maana yake ni kuwa kama mtu atakataa kumtumikia Yesu, basi atakuwa na deni kubwa la kulipa. Maisha yake yote yatakuwa katika moto. Tena akasema kama kuishi kwa ajili yake kutaleta kifo, basi malipo yake yatakuwa ni uzima wa milele.

Kristo alitupa sisi uhai ili tuishi kwa ajili yake. Mtu mmoja alisema "Upendo katika moyo wako haukuwekwa ili ukae tu. Upendo si upendo hadi utakapoutoa kwa watu wengine." Yesu hakufanya wokovu (ambao ni upendo wa



SURA YA KWANZA

# UUMBAJI WA MUNGU - KUANGUKA KWA MWANADAMU

Kusudi la Somo Hili: Nitafikiria maana ya dhambi.

Somo Kutoka: Mwanzo 1:26-31; 3

Vifungu vya Leo: Mwanzo 1:26-31; 3:1-13

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana..." (Mwanzo 1:31).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Sara alianza kuwaangalia rafiki zake wote waliokuwa mle darasani. Kila mmoja alikuwa akifanya mtihani uliokuwa mbele yake. Hapo alianza kukumbuka alipoingia katika shule ile kwa mara ya kwanza. Alipoingia kwa mara ya kwanza alijawa na furaha sana. Madarasa mazuri pamoja na rafiki zake walimfurahisha. Aliyapenda masomo yake, lakini sasa mitihani imeanza. Alifahamu ya kuwa ni lazima afanye vizuri kuliko wengine au hataweza kuipata ile kazi anayoipenda. Je, akishikwa anadanganya katika mtihani atapatwa na jambo gani? Moyo wake ulipiga upesi alipokumbuka kishawishi kile.

Rafiki yake alikuwa amemwambia, "Ninayo karatasi ya mtihani. Tunaweza kuisoma pamoja. Hakuna mtu atakayetugundua. Ebu fikiria tu jinsi wazazi wako watakavyofurahi kama utapata nafasi ya kwanza."

"Sara, unaumwa?" Mwalimu alimwuliza ili kuyarudisha mawazo yake darasani. "Hapana," alimjibu kwa kusitasita.

"Mimi ni mzima." Alijifikiria, "Kwa nini nilimsikiliza yule rafiki yangu?"

Je, Sara ni kama Hawa katika bustani ya Eden?

**Maelezo**

Adamu na Hawa waliishi kwa furaha katika Bustani ya Edeni. Tunasoma katika Mwanzo 1 ya kuwa walikuwa na kila kitu walichohitaji. Chakula pamoja na maji vilikuwa vingi. Pia Mungu alikuwa amewapa mamlaka juu ya vitu vyote ambavyo yeye alikuwa ameviumba. Woga wala magonjwa havikuwepo. Maisha yao yalikuwa shwari kabisa.

Mungu aliwabariki Adamu na Hawa kwa kuwapa kazi zao. Walitumia muda wao kama ilivyowapasa katika kuitunza bustani.

Jambo muhimu kuhusu bustani ile ni kuwa Mungu alikuwa pamoja nao. Walikuwa na ushirika mzuri sana pamoja naye.

Hata huko mbinguni, mahali pakamilifu, Shetani alipata njia ya kuingia. Alianza na majivuno. Mungu alikuwa amewapa Adamu na Hawa ruhusa ya kutumia bustani yote isipokuwa mti wa mema na mabaya (Mwanzo 2:17). Nyoka yule mwerevu akamwuliza Hawa, "Ati! hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile matunda ya miti yo yote ya bustani?" Alianza kuwapa wasiwasi.

Katika Mwanzo 3:1-6 tunasoma habari za kuanguka kwa mwanadamu. Shetani alimshawishi Hawa kula matunda yaliyokatazwa ambayo aliwaambia yatawafanya wawe werevu, tena wawe sawa na Mungu. Alikula lile tunda lakini jambo hilo halikumfanya atosheke. Alimpelekea Adamu tunda lile, naye pia akala. Hapo naye alimwasi Mungu.

Adamu na Hawa waliona aibu kwa sababu ya dhambi yao. Kwa mara ya kwanza walimwogopa Mungu. Katika



SURA YA KUMI NA TATU

# MSALABA NA MAISHA YA KIKRISTO

Kusudi la Somo Hili: Nitajifunza jinsi nitakavyoishi kwa ajili ya Kristo kila siku.

Somo Kutoka: Marko 8:34-38; 1 Petro 2:20-25; 4:12-19

Vifungu vya Leo: Marko 8:34-38

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "...Mtu ye yote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike na msalaba wake, anifuate" (Marko 8:34).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Mwalimu alianza kueleza, "Hapo zamani kulikuwepo na chungu cha kupikia ambacho kilikuwa kichafu sana. Chungu hiki kiliitwa mwanadamu. Kila mara kilikuwa kimejaa kitu hiki au kile. Hata yeye mwenyewe alipenda awe katika hali hiyo hiyo ya kujaa. Alijiona amejitosheleza yeye mwenyewe na mahitaji yake yote wala hakuwa na nafasi ya kitu kingine cho chote.

Siku moja Kristo alikutana na chungu hiki kilichojaa na kumweleza ya kuwa alikuwa na kitu fulani cha kumpa. Lakini kile chungu kilikuwa kimejaa sana wala hakikuhitaji kitu kingine cho chote. Mwanadamu alipotambua ya kuwa angepewa uzima wa milele alihuzunika kwa sababu alijiona ya kuwa ametosheka na mwenye uchafu mwingi hata hakuwa na nafasi ya kitu kingine cho chote."

Yule mwalimu alisisitiza ya kuwa Mungu hawezi kumtumia mtu ambaye amejaa majivuno wala mtu ambaye

Yesu ulifunuliwa wazi kwa wanafunzi hata walikuwa tayari kufa kwa ajili ya huo ujumbe. Na wengi wao walikufa kwa ajili hiyo.

Yesu alimshinda Shetani alipokuwa pale msalabani. Mungu na Shetani walikutana. Yesu alipata ushindi wa dhambi, uovu na kifo.

Kuna njia mbili ambazo Mungu angeweza kupinga dhambi. Angeweza kumwadhibu yule mwenye dhambi au kumwokoa mkosaji. Mungu aliamua kumwokoa mkosaji kwa njia ya Mwanawe. Katika Yohana 10:17-18, Yesu anasema ya kuwa hakuna mwanadamu ambaye angeweza kumlazimisha kufa. Alikufa kwa kupenda yeye mwenyewe. Pia kwa nguvu zake aliweza kuwa hai tena. Hilo ndilo lililotokea Yesu alipofufuka. Yesu alifufuka yu hai tena, naye alipaa mbinguni na kukaa mkono wa kuume wa Mungu, yaani Baba.

**Kazi ya Kufanya**

Fikiria haya yafuatayo na kuyatafakari au kwa kuandika majibu yake.

1. Hivi ungejisikia vipi kama ungeshuhudia mwalimu uliyempenda sana akiuwawa kama mwizi?
2. Kwa nini wanafunzi walionyesha wenye kukata tamaa?
3. Kwa nini hata wale ambao hawakuwa wafuasi wa Kristo walifadhaika aliposulubiwa msalabani?
4. Je, Yesu aliufanyaje msalaba kuwa ushindi?
5. Taja njia mbili ambazo Mungu alishughulikia dhambi.
6. Yohana 10:17-18 ina maana gani kwako?
7. Yesu alituahidi ya kuwa Roho Mtakatifu atakuja. Je, ahadi hii inawahusu Wakristo wa leo kwa njia gani?





Mwanzo 3:7-13, Mungu aliwauliza Adamu na Hawa kuhusu dhambi yao. Hata hivyo Adamu hakuwa tayari kukubali tendo lake alilotenda. Alimlaumu Hawa kwa kumpa lile tunda. Hawa naye alimlaumu nyoka.

Adhabu waliyopata Adamu na Hawa kwa ajili ya dhambi yao ilikuwa ni kufukuzwa nje ya bustani ile. Huo ulikuwa mwisho wa maisha makamilifu katika paradiso. Maisha yalianza kuwa magumu pamoja na mateso mengi. Nyoka naye alilaaniwa ya kuwa atatembea mavumbini milele.

Ndipo Mungu alipowatengenezea Adamu na Hawa nguo za ngozi za wanyama na kuwavika. Dhambi ilifanya damu ya wanyama imwagike. Baadaye tutajifunza kuhusu kafara ya damu ambayo watu walitoa kama sehemu ya ibada hadi wakati kafara kamilifu ya damu ya Yesu Kristo ilipolifanya tendo hilo lisiwe la lazima tena.

**Mafunzo Ya Sura Hii Kwangu**

Tunapaswa kutambua ya kuwa majaribu ya kutenda dhambi ni jambo ambalo ni la kweli katika maisha ya leo. Aina za majaribu hubadilika tunavyokua. Mtoto mdogo anaweza akawa anataka peremende. Kijana yeye matumaini yake ni kufanikiwa na kupata utajiri. Mtu wa umri wa makamu matumaini yake ni kuwa mtu mwenye madaraka. Shetani anatujaribu katika njia yo yote awezayo. Anatujaribu ili tuseme uongo au tuwaonee wivu Wakristo wengine na kwa njia hiyo anavunja ushirika wetu wa Kikristo tulionao. Anaweza akatujaribu tusitii wenye mamlaka, tukadanganya, tukaiba au kusengenya watu wengine.

Kama ilivyo katika hadithi hii yetu ya Sara, wanafunzi wanapaswa wapate alama za juu. Shetani atatumia nafasi kama hiyo ili aharibu njia zetu za Mungu.

Kuhusu Hawa, alikuwa na tamaa katika mambo matatu: alikuwa na tamaa katika mwili wake, kijicho na kujipenda. Alikiona chakula (jambo la kimwili), kuwa kilipendeza macho (tamaa ya macho) na kuwa kitamfanya mtu kuwa mwerevu (tamaa ya kujipenda au majivuno katika maisha). Soma Mwanzo 3:6.

Hivi leo labda tamaa zako zinaweza zikawa ni kwa vitu vya kukufurahisha kimwili kama uasherati au chakula. Vitu vyenye uzuri, nguo na magari hushawishi tamaa ya macho yetu. Mafanikio na majivuno mara kwa mara hutujaribu.

Kila tunaposhindwa na dhambi tuna deni ambalo tutalipa. Aliyetenda dhambi huaibika na kuwa mwoga mbele za Mungu. Hukataa kukubali kosa lake. Hapo anakuwa amekwisha kutengana na Mungu na anahitaji Mkombozi.

Tangu wakati wa dhambi ile ya mwanzo, mpango wa Mungu ulikuwa ni kumkomboa mwanadamu. Mungu katika upendo wake na msamaha atatuokoa kama alivyoliokoa taifa lake la Israeli kutoka utumwani. Aliwaokoa watu wake kutoka kuonewa na kutoka katika mateso.

Katika Agano Jipya kukombolewa ni kama deni. Mwanadamu amefungwa chini ya laana ya dhambi. Ni lazima malipo yawepo ili laana hiyo ipate kuondolewa. Deni hilo ni Mwana wa Mungu, Yesu Kristo. Alilipa deni la mwanadamu na kumwezesha mwanadamu kuwa huru kutokana na laana ya dhambi.

**Kazi ya Kufanya**

1. Nini wazo lako kuhusu paradiso? Kama ungeishi huko; Je, unafikiri ungejaribiwa na vitu vingine vya ajabu? Kama ndiyo, vitu vipi?

2. Je, unafikiri Adamu na Hawa walipofanya dhambi Mungu alijali? Je, atajali ukifanya dhambi.





Yesu aliwaambia ya kuwa kwa sababu atarudi kwa Baba yake, Mfariji mkuu, yaani Roho Mtakatifu atakuja kwao. Kwa njia hiyo, watu watakuwa na uwezo wa mambo mbali mbali vizuri zaidi kwa sababu Roho Mtakatifu yupo ndani yao. Lakini Yesu alipokuwa anaishi na wanafunzi wake, wao hawakuyaelewa mambo haya.

Katika sura ya 23:48-49, Luka ameeleza jinsi wanafunzi wake walivyojisikia. Wanafunzi wake waliposhuhudia kile kitendo cha kusulubiwa msalabani walifadhaika sana. Wala hawakuweza kukumbuka maneno ya kutia moyo ambayo Yesu alikuwa amewaeleza kabla ya kufa kwake. Walijisikia wameachwa pweke na waliingiwa na hofu kwa maisha ya baadae. Baada ya kutojua la kufanya, walirudi nyumbani kwao. Wote walibaki katika hali ile ya kufadhaika mpaka wakati Mariamu Magdalene alipotangaza kwa furaya ya kuwa, "Kaburi liko tupu. Lile jiwe limeondolewa!" Luka ameandika yale aliyoyaona katika Luka 24:13.

Tumaini la wale wanafunzi liliongezeka baada ya kusikia habari za Mariamu. Hata Yesu alipowatokea ilihakikisha yale waliyokuwa wanafahamu. Kristo amefufuka!

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Kama ilivyokuwa siku ile ya kwanza ya sabato kuwa ishara ya msalaba sio kushindwa, ndivyo ilivyo hata leo. Msalaba ulileta ushindi. Ni ushindi kwa wale wanaokubali mpango wa Mungu. Wanafunzi walianza kuelewe ya kuwa Roho Mtakatifu hawezi kuwajia mpaka Yesu apae mbinguni. Huyu Roho Mfariji atakapokuja, yeye ndiye atakayewaongoza na kuwalinda katika utumishi wao. Hata leo hiyo ndiyo kazi ya Roho Mtakatifu, katika maisha ya kila mwamini.

Kifo cha Yesu pale msalabani kilimletea kila Mkristo ushindi. Kila jambo lilifunuliwa wazi. Kwa kweli ujumbe wa

gazeti. Shule moja kati ya hizo ilitangaza nafasi za elimu kwa wakimbiaji. Yohana alikuwa amekuwa mkimbiaji hodari hata kuweza kuishinda ile hali yake ya kulemaa iliyotokana na kupooza.

Kwa kujitahidi sana, Yohana aliongeza sana mbio zake. Aliweza kuwa wa kwanza kuukata ule utepe wa kumaliza mbio. Ushindi ulikuwa wake!

**Maelezo**

Mtu anayeshinda hupendwa na kila mtu. Watu wengi hupenda washinde. Wale wafuasi wa Kristo walipomwangalia akiwa pale msalabani hawakuwa na matumaini ya kuwa atashinda. Kwa wengi hilo lilikuwa ni janga kubwa siku ile.

Kwa sababu ya kuomboleza kwa ajili ya kushindwa kwao, na hata mioyoni mwao walijawa na huzuni. Walitaka wajifiche. Yuda Iskariote alikuwa amekwisha kufa. Alikuwa amejinyonga kwa sababu ya kumsaliti Bwana wake. Petro alikuwa ameingiwa na hofu kubwa. Alikuwa amemkana Yesu mara tatu. Wote walikuwa bado wanakumbuka kusulubiwa kwake na ukatili wa kitendo hicho. Yesu alipokuwa pale msalabani, watu walianza kumshutumu. Makuhani na waandishi walimdhihaki. Watu wengi waliokuwa wanapita karibu na mahali hapo walikuwa wanatikisa vichwa vyao.

Wafuasi wa Yesu walikuwa wakiangalia. Walikuwa wamekata tamaa. Masihi wao alikuwa amekufa. Tumaini la kuishi halikuwepo tena. Sasa watafanya nini?

Soma katika Yohana 16:5-16 jinsi Yesu alivyokuwa anawaeleza kuhusu mambo yatakayo kuja. Yesu alifahamu kuwa wanafunzi wake hawakuelewa kuhusu kifo chake. Aliwaambia mambo hayo ili baadaye waweze kuyatafakari na kuyaelewa.





3. Ni kitu gani kinachotufanya tutende dhambi?
4. Ni dhambi zipi zinazotutenganisha na Mungu?
5. Mungu alilipa gharama gani katika kuondoa deni letu la dhambi?
6. Tutawezaje kuwa huru kutokana na mzigo wa dhambi? (Soma Yohana 3:16.)

SURA YA PILI

# ASILI YA DHAMBI

**Kusudi la Somo Hili:** Nitafikiria kuhusu uhuru wangu wa kumtii au kutomtii Mungu.

Somo Kutoka: Mwanzo 6

Vifungu vya Leo: Mwanzo 6

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Ndivyo alivyofanya Nuhu, sawasawa na vyote alivyomwamuru Mungu..." (Mwanzo 6:22).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Uovu ulijaa katika kile chumba cha disco. Sauti ya vicheko ilisikika kwa juu zaidi kuliko ile ya muziki uliokuwa unapigwa. Sherehe hiyo ilikuwa imeanza saa nne kabla ya muda wake. Unywaji ulianza maru tu baada ya wageni kufika. Yusufu alijisikia ya kuwa anaumwa. Kwa sababu ya moshi wa sigara katika kile chumba kupata hewa nzuri kulileta shida nyingi. Samweli alikuwa amemshawishi ya kuwa sherehe kama hizo ndizo alizohitaji ili aweze kubadilisha ile hali ya uchovu wa maisha aliokuwa nao. Alimwambia ya kuwa, "Unatakiwa ukutane na wasichana wenye kupendeza."

Yusufu aliangalia pale walipokuwa. Alijisikia kama anataka kutapika. "Nitajiaibisha mimi mwenyewe kama sikutoka mahali hapa haraka iwezekanavyo. Alijiuliza, "Kwa nini nilijitakia sherehe kama hii?"

**Maelezo**

Katika sura ya kwanza tumejifunza ya kuwa dhambi iliingia duniani wakati Adamu na Hawa walipokubali vishawishi vya nyoka katika Bustani ya Edeni.



SURA YA KUMI NA MBILI

# MSALABA NI USHINDI WA DHAMBI

Kusudi la Somo Hili: Nitajifunza jinsi ambayo msalaba unaweza kufanya maisha yangu yawe ya ushindi.

Somo Kutoka: Yohana 16:5-16; Luka 23:48-49; 24:3

Vifungu vya Leo: Yohana 16:5-16

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Na yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo nalisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo yangu, na kuwapasheni habari" (Yohana 16:15).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Kimbia! Kimbia! Kimbia! Hizo zilikuwa ni sauti za washangiliaji. Kila mtu aliyekuwepo alimshangilia ili apate ushindi.

Haya hayakuwa ni mashindano ya kombe la dunia. Kusudi la mbio hizi lilifahamika tu kwa kijiji kile.

Yohana alikuwa mtoto wa tano kati ya watoto wanane katika jamaa yake. Kila wakati maisha yake yalikuwa katika matatizo. Alipokuwa mtoto mdogo aliugua sana. Homa kali iliyompata ilimfanya aweze kupooza kwa muda. Baada ya kupona, siku moja akiwa anacheza, rafiki yake alimpiga kwa jiwe jichoni. Ajali hiyo ilifanya jicho lake lisiweze kuona vizuri. Pia kila mara alikuwa hana fedha za kutosha kwa kulipia ada ya shule. Baada ya kumaliza darasa la sita, ilimbidi aanze kutafuta kazi.

Mbio hizi ndizo zingempa nafasi ya kwendelea na shule. Yohana alikuwa amesoma kuhusu mashindano hayo katika

5. Uamuzi wako kuhusu Yesu ni upi?

6. Omba ili upate hekima ya kumfahamu Mungu. Katika Yakobo 1:5-7, Mungu ameahidi ya kuwa yeye atatoa pasipo kukemea. Imani ndio ufunguo kwa majibu ya Mungu.

7. Ombea mambo yafuatayo: Kama unakubaliana nayo, basi andika jina lako na tarehe hapo chini.

Nataka nimfahamu Mungu zaidi. Kwa hivyo kwa msaada wa Mungu, najitoa katika kuomba na kusoma Biblia kwa dakika 15 kila siku.

JINA________________ TAREHE __________





Kwa sababu Mungu anampenda mwanadamu, alitayarisha mpango wa kumwokoa mwanadamu kutokana na dhambi aliyoamua kuitenda. Ukweli ni kuwa mwanadamu hakulazimishwa kutenda dhambi. Alikuwa na haki ya kufanya uamuzi. Mungu alimpa mwanadamu uwezo wa kufanya uamuzi kwa ajili yake yeye mwenyewe. Mungu aliumba kila mtu ili awe na uwezo wa kujifikiria yeye mwenyewe. Kwa ajili ya uhuru huu wa kujiamulia, Adamu na Hawa waliamua kutenda dhambi kinyume cha maagizo ya Mungu. Kwa ajili hiyo dhambi iliingia duniani. Sasa lazima tuangalie nini maana ya dhambi.

Katika Mwanzo 6:5-7, tunasoma kuhusu siku za Nuhu. Katika vifungu hivi inaonekana ya kuwa Mungu alikuwa amechoshwa na dhambi duniani. Biblia inatuambia ya kuwa Bwana aliuona uovu kila mahali, ingawa mwanadamu alifurahia uovu wake.

Katika kuhuzunishwa na jambo hilo, Bwana alisema ya kuwa ataiharibu dunia. Mwanzo 6:8-11 inatupa dalili za matumaini. Katika uamuzi wake huo wa kuhuzunisha wa kuiharibu dunia, tumaini lilionekana. Mungu alimpata mtu hapa duniani ambaye alimpenda na kumtii yeye.

Biblia inatuambia ya kuwa Nuhu alipata kibali mbele ya macho ya Mungu. Nuhu alikuwa mtu mwenye haki naye alikuwa hana dosari wakati wa kizazi chake.

Alitembea na Mungu. Mungu alimbariki Nuhu naye akawa na watoto yaani Hamu, Shemu na Japheti.

Aina yote ya uhai duniani ingeangamizwa isipokuwa Nuhu, watoto wake na familia zao. Pia Mungu aliwaokoa wale wanyama aliomwambia Nuhu awaweke katika safina.

Katika dunia yenye kuteketea, Mungu aliamua aokoe sehemu ya kile alichokiumba kisiharibike kabisa. Kwa

kumwokoa Nuhu, na vile viumbe vingine katika safina, Mungu alikuwa amewaruhusu wanadamu waendelee kuishi.

Dhambi ni nini? Katika maneno rahisi dhambi ni kuasi mapenzi ya Mungu. Ni uovu ule ambao unavunja ushirika wetu na Mungu.

**Mafunzo Ya Sura Hii Kwangu**

Mwanadamu ameumbwa kwa sura ya Mungu. Kwa ajili hiyo, mwanadamu anao uamuzi. Yeye anao uwezo wa kutii au kutotii.

Mwanadamu ni tofauti na wanyama kwa sababu anao uwezo wa kufikiri. Anaweza kutumia maarifa aliyonayo kwa lengo la kujiendeleza yeye mwenyewe. Lakini mnyama anategemea tu silika yake tangu asili. Tunaweza kuwatawala wanyama kutokana na chakula ambacho bwana wake atawapa. Wakiwa wameshiba vizuri wanafurahi. Lakini mtu sivyo, yeye hufurahi wakati anapoweza kufanya uamuzi wake mwenyewe.

Mwanadamu anapoamua kutenda dhambi, anakuwa amefanya dhambi mbele za Mungu. Kama tutamruhusu Shetani kuharibu uamuzi wetu na kufuata mambo ya dunia, hiyo ni dhambi. Mwanadamu anapaswa kufahamu ya kuwa asifanye mambo fulani kwa sababu yeye ni Mkristo. Kama atajiunga na mambo hayo na kuyafurahia badala ya kuyakimbia anapowaona wengine wakiyafanya, ni dhambi ya kujitakia. Dhambi ya kujitakia ndiyo iliyowapata watu wakati wa siku za Nuhu. Dhambi kama hii bado watu wanayo kila siku. Baadhi ya dhambi hizi ni wivu, majivuno, uasherati na chuki.

Kila siku mwanadamu anakabiliwa na ukosefu wa imani. Huku ni kumkataa Mungu kama alivyofunuliwa kwa njia ya Yesu Kristo. Hii ni dhambi ya mauti. Imani katika Yesu,





Ebu fikiria uhusiano wa Mungu na msalaba wa Kristo. Msalaba ulikuwa wa lazima kwa sababu ya tabia ya asili ya Mungu na uhusiano wake na dhambi za wanadamu. Kwa sababu ya tabia ya asili ya Mungu, yeye hawezi kuvumilia dhambi za mwanadamu. Njia maalumu ilihitajika ya kumpatia mwanadamu namna ya kumrudia Mungu. Tena jambo hili halikuwa ni la ghafla tu. Ni jambo ambalo lilikuwa limepangwa tangu hapo mwanzo.

Je, daraja kati ya Mungu na mwanadamu ingeweza kuwa nini? Mungu angefanya nini na dhambi? Kwa vyo vyote hangeweza kuwatendea wenye haki sawa na wale wasio na haki. Jibu lake lilikuja kwa njia ya Kristo pale msalabani. Mwana wa Mungu alitolewa awe kafara wa kujenga daraja kati ya Mungu na mwanadamu mwenye dhambi. Yesu Kristo alikuwa mlango ulio wazi wa kumwendea Mungu. Kwa sababu Yesu alilipa deni kwa ajili ya dhambi za wanadamu, mwanadamu sasa anaweza kumwendea Mungu akiwa kama Mwanawe. Neema ya Mungu ipo juu ya sheria (ambayo ni njia ya kuiadhibu dhambi). Upendo wa Mungu wa kuokoa ndio uliomwonyesha mwanadamu njia ya wokovu.

**Kazi ya Kufanya**

Fikiria haya yafuatayo kwa kuyatafakari au kwa kuandika majibu yake.

1. Je, utamwelezaje Mungu?
2. Ni kitu gani kinachokuja katika akili yako unapofikiria kuhusu utakatifu?
3. Je, Mungu anajisikiaje kuhusu dhambi? Je, anaweza kuvumilia dhambi?
4. Kwa nini Mungu alimruhusu Mwanawe afe kwa ajili ya mwanadamu mwenye dhambi?

Kutokana na mafundisho ya Yesu, tumefunuliwa ubaba wa Mungu, kama vile watoto wanavyohusiana na baba yao wa duniani. Tofauti kati yao ni kuwa Mungu ni mkamilifu na uhusiano wake wote na wengine ni mzuri. Ila mwanadamu anaweza kufanya maovu, hata kwa watoto wake mwenyewe. Baba wa duniani anaweza kufanya makosa, lakini Mungu ni mkamilifu katika mambo yote.

Mungu huwamwagia watoto wake upendo wake wa kibaba. Ni mapenzi yake kuwa wote waokolewe. Soma Mathayo 18:14. Hapa ndipo tunaona umuhimu wa uhuru wa mwanadamu katika kutimiza mapenzi yake. Mwanadamu huchagua njia yake mwenyewe. Mwanadamu anachagua kutaka au kutotaka katika kuyafuata mapenzi ya baba.

**Mafunzo Ya Sura Hii**

Katika sehemu hii ndipo palipo na umuhimu katika kujifunza somo hili. Ni lazima kujifunza tabia ya Mungu ili tuweze kuelewa uhusiano uliopo kati ya Mungu na msalaba wa Kristo.

Mungu ni upendo. Bila shaka hapa ndipo tunapopata tabia hasa ya Mungu. Upendo huu sisi hatuwezi kuueleza. Upendo ambao mwanadamu anaufahamu ni ule wa kawaida wa jamaa na marafiki. Upendo wa Mungu si kitu cha kujisikia tu (au hisia) peke yake basi. Unahusisha maisha yote kwa ujumla. Ni mkusanyiko wa sheria na neema, yaani mambo ya kufuata, lakini vile vile una karama ya uzima wa milele ambayo ni bure.

Mungu ni mwenye haki. Mungu wa Agano la Kale na Mungu wa Agano Jipya hangeweza kutoangalia dhambi. Yeye hatavumilia kuona ya kuwa sheria zake zinavunjwa.

Tabia nzima ya Mungu, tunaweza kuiita kuwa ni upendo au haki ambayo ni kazi ya wokovu.





Mwana wa Mungu, huleta uzima wa milele katika Mungu. Kutokuamini kunaleta kifo. (Warumi 6:23).

Mwanadamu anakabiliwa na moyo mwovu kila wakati. Katika Marko 7:14-23, Yesu alisema ya kuwa dhambi ipo nje na ndani. Maana yake ni kuwa, mtu anaweza kutenda dhambi katika moyo wake kama vile anavyoweza kutenda dhambi kwa matendo yake. Biblia inatuambia ya kuwa tunakuwa tumemkosea ndugu yetu katika moyo wetu kwa kumtakia kitu kama kifo. Yohana anaendelea mbele hatua moja zaidi kwa kusema ya kuwa, "Kila amchukiaye ndugu yake ni mwuaji..." (1 Yohana 3:15).

Pasipo Yesu mwanadamu yuko chini ya vifungu vya dhambi. Mwanadamu hawezi kujiokoa yeye mwenyewe kutokana na nguvu za dhambi. Pasipokuwa na nguvu za kuokoa za neema ya Mungu, mwanadamu atazidi kudidimia katika dhambi.

Mungu amempa kila mmoja uhuru wa kutii au kutotii. Je, umekuwa huru kutoka katika vifungo vya dhambi? Kama bado, je, utamwamini Yesu na kupokea uhuru ambao yeye anakupa leo hii?

**Kazi ya Kufanya**

Andika au jadilianeni majibu ya maswali yafuatayo:

1. Linganisha maisha ya Adamu na Hawa kabla ya kumwasi Mungu na baada ya kumwasi Mungu.

2. Dhambi ya kujitakia ni ipi?

3. Orodhesha baadhi ya mambo unayojisikia wakati unapoamua kutenda kwa makusudi jambo ambalo sio sawa.

4. Je, maisha yako yangekuwa namna gani kama hungeweza kuwa huru kufanya uamuzi wako mwenyewe kuhusu jambo jema au baya.

5. Soma Marko 7:14-23. Jadilianeni kuhusu mambo maovu ambayo tunaamua sisi wenyewe yatuharibu. Kwa nini unafikiri tunafanya hivyo?

6. Kwa nini unafikiri Mungu alikupa uwezo wa kuamua wewe mwenyewe?

7. Kama hujaamua kuchagua uhuru unaotokana na kumtumaini Yesu kama Mwokozi wako, je, utafanya uamuzi huo leo?





**Maelezo**

Je, Mungu ni kama nani? Je, anafahamu ya kuwa mimi naishi? Je, nitawezaje kumfahamu vizuri zaidi? Wengi wetu tumekuwa tukitafuta majibu ya maswali haya. Kwa kujifunza maandiko ya Biblia, tutaweza siku hii ya leo kumwelewa Mungu zaidi.

Kitabu cha Zaburi tunachokisoma kiliandikwa na Daudi. Kinatusaidia kuelewa jinsi Daudi mwenyewe alivyomwelewa Mungu. Katika vifungu vya 1-6 vya Zaburi 19, Daudi anausifu utukufu wa Mungu. Anaeleza ya kuwa aliweza kumwona Mungu kila mahali. Daudi alimwona Mungu akiwa yuko juu ya vyote. Hakuna mtu ambaye angeweza kuumba mbingu na nchi isipokuwa Mungu. Katika vifungu vya 7-10, Daudi anaeleza hisia zake Mungu. Tafadhali visome kwa uangalifu. Pia soma Zaburi 89:5-18 ili uweze kupata mawazo ya mtu mwingine kuhusu Mungu.

Ni jambo rahisi kuona jinsi Mungu alivyopewa heshima na waandishi wote hawa. Wameweza kuonyesha ya kuwa Mungu anayo busara zaidi kuliko mzee mwenye akili nyingi. Sio tu kuwa yeye amekalia kiti cha enzi huko mbinguni. Wala hakujitenga kabisa na ulimwengu unaomzunguka.

Vifungu hivi vya Biblia vinatuonyesha ya kuwa Mungu ni mkamilifu. Yeye ni mwenye haki, tena ni Mungu wa kweli mwenye upendo na uaminifu. Vitu vyote viko chini yake. Kwa njia hii tunaweza kumwelewa Mungu tabia yake na uhusiano wake na msalaba wa Kristo. Kwa nini ilimbidi Yesu afe msalabani? Je, msalaba wa Yesu utawezaje kumwokoa mtu? Msalaba huu utakuokoaje wewe na mimi? Katika majibu ya maswali haya ndipo palipo na uhusiano wa Mungu, ambaye ni Baba Mtakatifu, pamoja na Mwanawe na hata wanadamu wengine wote.

SURA YA KUMI NA MOJA

# MSALABA NA TABIA YA MUNGU

Kusudi la Somo Hili: Nitaazimu ya kuwa nitatumia dakika 15 katika sala kila siku na kusoma Biblia ili niweze kumwelewa Mungu vizuri zaidi.

Somo Kutoka: Zaburi 19; 89:5-18

Vifungu vya Leo: Zaburi 19

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono yake" (Zaburi 19:1).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Mara nilijikuta niko macho. Moyo wangu ulikuwa unapigapiga kwa nguvu. Kuhema kulikuwa shida. Je, ni kweli nimesikia sauti ya Mungu? Nilianza kuwaza kuhusu ndoto iliyoniamsha katika usingizi.

Nilikuwa nimesimama mbele za Mungu. Woga wa kuhukumiwa kwa ajili ya dhambi zangu ulinifanya nitetemeke. Nilipoyafungua macho yangu taratibu, niliweza kuuona uso wa Mungu. Aliniangalia kwa macho yaliyojaa upendo. Wasiwasi ulinitoka na nilijiona niko salama.

Wewe unamwamini Mwanangu, yaani Yesu. Umejifunza neno langu, zaidi ya yote umeishi kutokana na yale uliyojifunza. Hivyo ni vizuri sana, wewe ni mtumishi mwaminifu. Njoo uishi nami milele."

Kama alivyokuwa yule mtoto mpotevu, nilikumbuka jinsi nilivyomkimbilia yeye, yaani Baba yangu mpendwa.

Machozi yalinijaa machoni na nilijisikia nimejawa na upendo wake. Hivi kweli hiyo ilikuwa ni ndoto?



SURA YA TATU

# MSHAHARA WA DHAMBI

Kusudi la Somo Hili: Nitajifunza kile kinachotokea dhambi inapoingia katika maisha.

Somo Kutoka: Warumi 1:18-32; 6:23

Vifungu vya Leo: Warumi 1:18-32

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Warumi 6:23).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Mlango wa gereza ulifungwa kwa nguvu na sauti yake ikaingia masikioni mwa Tomasi. Huu ulikuwa ndio mwisho wa safari yake ya dhambi. Jambo lo lote baya lilipotokea hakuliona kuwa baya. Kitendo cha kutumia fedha ovyo ovyo alikiona kuwa kilikuwa rahisi. Karani wa hesabu alipogundua wizi wake, alipaswa auawe. Kifo ni jambo ambalo kwa Tomasi lilionekana dhahiri.

Alikuwa anapenda sana maisha ya anasa. Yeye alifikiria ya kuwa ni lazima awe na gari la Mercedes, awe na nyumba kubwa au awapeleke watoto wake katika shule nzuri nzuri na kadhalika. Tomasi hakuamini ya kuwa hayo yote sasa yamekwisha. Hukumu ya hakimu itakuwa ya mwisho. Sasa atakufa kwa sababu ya tamaa zake.

**Maelezo**

Kwa kuwa asili ya dhambi ni kutomtii Mungu kwa kujitakia, kwa hakika dhambi inayo matokeo yake. Mungu

ni Mungu mwenye haki. Matokeo ya dhambi ni kutengana na Mungu.

Mtu anapotenda dhambi ni lazima ategemee kuvuna matokeo ya dhambi. Tokeo moja laweza kuwa ni kujiona mwenye hatia kwa muda mrefu mpaka utakapopatana na Kristo. Wakati mwingine mtu huyu anaweza akashikwa katika tendo la dhambi na kupewa adhabu.

Kila mara dhambi ina matokeo yake, hata kama huyu mtu atashikwa au asishikwe katika tendo la dhambi. Pia kila mara kuna haja ya wokovu kwa njia ya Yesu Kristo.

Ghadhabu ya Mungu ipo wazi katika Warumi 1:18-25. Soma vifungu hivyo. Kwa mara nyingine tena Mungu alikuwa anakabiliwa na watu wasiomcha. Walifahamu ya kuwa walikuwa wakitenda mabaya. Hata watu wao wenyewe walimfahamu Mungu na haki yake, lakini waliendelea katika dhambi zao. Sanamu walizozitengeneza wanadamu zilikuwa badala ya Mungu.

Nyakati zile hawakuogopa kutumia miungu ya sanamu. Walijiona ya kuwa walikuwa watu wenye hekima lakini kwa kweli walikuwa wajinga. Walifahamu ya kuwa yale ambayo walikuwa wakifanya yalikuwa kinyume cha mapenzi ya Mungu, ila waliendelea tu kufanya hivyo. Walikuwa watu wenye uchoyo na walitaka tu kutimiza mahitaji yao. Hawakuwa na muda kabisa wa kumfikiria Mungu na sheria zake.

Warumi 1:26-32 inatuambia kwa wazi kile ambacho watu walikuwa wakifanya. Vifungu hivi vinatuonyesha kwa wazi kile ambacho kwa Mungu ni dhambi. Uovu wa kila aina kwa Mungu na asili yake ulikuwa unafanyika. Wakristo wote leo hii wanaelewa matendo yote yaliyo katika vifungu hivi ya kuwa ni maovu.





5. Je, utamwelezaje habari za Yesu mtu ambaye hajasikia habari zake?

6. Je, unadhani inawezekana kwako wewe kuishi maisha ya upendo yenye kuwajali wengine? Kama ndiyo, kwa nini? Kama sivyo kwa nini?

7. Je, wiki hii utafanya nini ili uweze kuwa kama Yesu zaidi?

dhambi. Hata alipokuwa akiteswa hakurudisha ovu kwa ovu.

Imeelezwa mara nyingi kuwa 1 Wakorintho 13 ni maelezo ya Yesu. Maandiko yanatueleza "Mungu ni pendo". Upendo wa kweli ulionekana pale msalabani. Upendo kamili unaeleza chanzo cha Yesu Kristo. Leo anatawala milele katika ufalme wake. Yeye aliondoa vikwazo vyote ili mwanadamu aweze kupata njia ya kumwendea Mungu.

Je, wewe umemwendea? Je, umempokea Yesu kama Mwokozi wako? Je, unaweza kufanya nini ili uweze kuufuata upendo huo kamili? Kifungu chetu cha kukumbuka kinatupa mwanga: ni kujitoa kabisa kwa Yesu awe kama Bwana. Jambo hili si rahisi, wala hatuwezi kulifanya sisi wenyewe. Mungu ametuahidi yule Roho Mtakatifu kama kiongozi wetu kila mara. Soma katika Yohana 14:18.

Kubali leo kufuata mfano wa Yesu katika maisha yako ya kila siku.

**Kazi ya Kufanya**

Fikiria maswali yafuatayo kwa kujadiliana au kwa kuandika majibu yake.

1. Yesu alijishughulisha na mahitaji ya wanadamu alipokuwa hapa duniani. Je, unaweza kutaja baadhi ya miujiza yake ambayo anatuonyesha ya kuwa yeye alitujali sana?

2. Jadilianeni baadhi ya mafundisho ya Yesu ambayo yanatuonyesha ya kuwa yeye aliwajali wanadamu.

3. Tutaweza kujifunza nini kutoka kwa Yesu jinsi tutakavyoweza kuishi leo?

4. Kuishi kwa kufuata mfano wa Yesu kutawezaje kubadili uhusiano wetu na jamii zetu? Na rafiki zetu wa Kristo? Na wale ambao si Wakristo?





Kila Mkristo anapaswa avisome vifungu hivi kwa makini. Maelezo yake yanatuelekeza yale yanayotokea wanadamu wanapomwacha Mungu na kuzifuata njia zao wenyewe za ubinafsi. Kama utayasoma maelezo hayo, basi kwa hakika kutakuwa na maswali yo yote katika mawazo ya Mkristo kuhusu maana ya kumkosea Mungu katika dhambi.

Mungu alisema ya kuwa watu hawa wanastahili kufa kwa sababu ya dhambi zao. Mungu alisema ya kuwa sio kuwa watu hawa waovu wanapenda dhambi, bali pia wanawakubali wale wanaotenda dhambi.

**Mafunzo Ya Sura Hii Kwangu**

Bila shaka jambo hili linawaambia Wakristo wa leo kuwa waseme kwa wazi, hasa wale ambao wanaendelea kuishi katika dhambi. Lazima pawepo na ushuhuda wa Kikristo katika kupinga matendo ya dhambi. Matendo kama hayo yasemwe yalivyo: yaani ni ya dhambi.

Ebu fikiria matokeo ya dhambi. Kwanza dhambi inatenganisha mwanadamu na Mungu. Dhambi inaweza kuonekana katika hadithi ya yule mtoto mpotevu. Hadithi hii inatuonyesha tamaa ya anasa na uovu wa dhambi. Dhambi maana yake ni kwenda mbali na Mungu. Inafanya mtu amwasi Mungu na kumwondoa Mungu katika maisha yake.

Je, unakumbuka ya kuwa Adamu na Hawa walijaribu kujificha ili Mungu asiwaone? Hata leo hii mtu anapofanya dhambi anajaribu kujificha ili Mungu asimwone, jambo ambalo kwa kweli haliwezekani.

Paulo anatueleza leo ya kuwa watu wa wakati huu hawakuacha dini zao, bali dini hiyo ilikuwa imepotoka sana. Watu walianza kuabudu sanamu. Walitengeneza vitu vingine badala ya Mungu. Hata leo hii watu wametengeneza vitu

vingine badala ya Mungu pia. Wengine wanatumia elimu, fedha, madaraka na vitu vingine kama Mungu wao. Watu wengi wanaabudu mali zao walizonazo hata wako tayari kulipa kitu cho chote ili wakipate hata ikiwa ni kuua.

Dhambi inamzuia mtu asimwabudu Mungu. Watu wanapofikiria ya kuwa wanaweza kuficha dhambi zao kwa kwenda kanisani kwa kweli wanajidanganya wao wenyewe. Mungu anayafahamu yote na atahukumu kwa haki.

Dhambi pia humdhalilisha yule mwenye dhambi. Inamzuia mtu asiwe na ushirika na Mungu, pia na Wakristo wengine. Hakuna mtu hata mmoja anayependa kusema ya kuwa amefanya dhambi, lakini kila mtu amefanya dhambi. "Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu" (1 Yohana 1:8).

Pia twapaswa kutambua ya kuwa dhambi huleta mateso. Wakati mwingine adhabu inamwangukia yule ambaye amefanya dhambi. Wakati mwingine inawaangukia wazazi, watoto, marafiki au kanisa.

Neema ya Mungu ilileta mpango mpya duniani wa kumsaidia mwanadamu. Huu ni mpango wa wokovu.

Kwa wazi Biblia imeeleza kabisa yakuwa dhambi huleta kifo. Tumaini letu lipo tu katika Yesu Kristo. Mungu anachukia dhambi ingawa anampenda yule mwenye dhambi. Kwa yule ambaye ni mwamini katika Kristo kuna wokovu kutoka dhambini kwa njia ya deni ambalo Yesu Kristo alilipa pale msalabani. Kwa wale ambao hawamkubali Kristo, kuna mateso ya milele. Uchaguzi ni wako.

**Kazi ya Kufanya**

1. Kwa nini dhambi lazima imtenganishe mtu na Mungu?
2. Warumi 6:23 ina maana gani inaposema, "Mshahara wa dhambi ni mauti"?





"...alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba." Kwa hiyo Mungu alimwadhimisha mno mwanawe hata akampa mahali pa heshima karibu naye.

Katika Agano Jipya kuna habari nyingi kuhusu uhai wa Yesu katika mwili. Soma katika Waebrania 2:18 ambayo ni maelezo kuhusu kujaribiwa kwa Yesu. Yeye kama mwanadamu alijaribiwa, kwa hiyo anaelewa kujaribiwa kwetu. Yeye atatusaidia tushinde kila jaribu. Soma kuhusu sala ya Yesu na mateso aliyopata alipokuwa anakabiliwa na kifo katika Waebrania 5:7. Maelezo kuhusu kuzaliwa kwake na maisha yake alipokuwa mtoto katika Mathayo na Luka yanatuonyesha jinsi alivyokuwa mwanadamu.

**Mafunzo Ya Sura Hii Kwangu**

Ebu jaribu kutafakari ukweli huu: Yesu alikamilisha unabii wa Biblia. Kifo chake kiliwaletea wanadamu wa kila umri, na kila taifa uzima. Maisha yake ya utumishi na upendo ni mfano ambao sisi sote twapaswa kuiga.

Yesu alipoishi hapa duniani alijishughulisha sana na mahitaji ya wanadamu. Alielewa ya kuwa twahitaji mahitaji haya kwa sababu naye pia alikuwa mwanadamu. Kutushughulikia kwake ni wazi tunaposoma miujiza yake mbali mbali ambayo aliifanya. Huruma zake ni wazi kwani aliwafanya vipofu waone na viwete watembee. Kwa kuwafufua wale waliokufa na hekima iliyokuwa katika mafundisho yake, alituonyesha ya kuwa yeye alikuwa Mungu.

Ukisoma 1 Petro 2:19-25 utaelewa ya kuwa kwa kweli Yesu hakustahili mateso aliyoyapata. Yesu alitimiza tendo lake la kuteswa kwa ajili ya wanadamu. Isaya, nabii, alimwita mtu mwenye huzuni nyingi. Tunaambiwa ya kuwa tufuate mfano wake ambao ametuonyesha sisi (1 Petro 2:21). Kifungu cha 22 kinatueleza ya kuwa Yesu alikuwa hana

"Je kutokana na kipimo cha Mungu, sisi tumefanikiwa kiasi gani? Labda kuna watu ambao wanazaliwa ili walipe deni kwa ajili ya kufanikiwa kwa watu wengine.

**Maelezo**

Tunafahamu ya kuwa Yesu Kristo alikufa msalabani ili awapatie wanadamu ukombozi. Tunaelewa pia ya kuwa mateso aliyopata Yesu pale msalabani yalikuwa makali zaidi kuliko ya mtu ye yote mwema ambaye amejihusisha na matatizo ya wanadamu.

Je, huyu Yesu ni nani hata alipe gharama kubwa kiasi hicho kwa ajili ya dhambi za wanadamu? Somo hili linatufundisha kwa nini Yesu alitimiza kusudi la Mungu la uzima wa milele.

Agano la Kale limejaa unabii kuhusu kuja kwa Masihi. Yesu Kristo alikamilisha kila unabii. Chanzo cha asili ya Bwana ni ukweli. Je, unafahamu unabii wo wote kuhusu Yesu? Yeye alizaliwa na bikira huko Bethlehemu. Aliishi ingawa mfalme mmoja aliyekuwa na wivu aliwaua watoto wachanga wote katika mji wake. Yesu alitimiza mambo yote haya.

Agano Jipya halikueleza historia ya watu wengi ambao wamejiita kuwa wao ni Masihi. Agano Jipya linatueleza habari za Masihi mmoja ambaye alituhakikishia ya kuwa yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Unabii wa Isaya ulikamilika wakati Yesu aliposulubishwa pasipo hata mfupa wake mmoja kuvunjika.

Yohana 1:1-3 inatueleza zaidi kuhusu nafsi ya Kristo. Yesu alikuwa pamoja na Mungu dunia ilipoumbwa. Vifungu vya maandiko vinamwita Yesu "Neno." Hilo Neno, yaani Yesu, alikuwa mwili naye akaishi kati ya watu, akiwa amejawa neema na ukweli. Katika Wafilipi 2:8, Paulo alisema,





3. Soma kifungu cha leo cha kukumbuka. Pia soma Warumi 6:21; 8:6 na Yakobo 1:15. Je, unaweza kutoa uamuzi gani kuhusu vifungu hivi?

4. Je, unawezaje kuishughulikia dhambi ambayo ipo katika maisha yako? Angalia vifungu vya 24-32 na uone kama yo yote kati ya dhambi hizo ipo katika maisha yako.

5. Je, unachagua au unakataa uzima wa milele katika Yesu Kristo.

6. Chunguza jambo hili: uzima wa milele ni karama ya bure kutoka kwa Mungu.

SURA YA NNE

# AHADI YA MUNGU YA MSAMAHA

Kusudi la Somo Hili: Nitamsamehe yule atakayeniudhi.

Somo Kutoka: Mika 7:18-19, Hesabu 14:18; 1 Yohana 1:3-10

Vifungu vya Leo: 1 Yohana 1:3-10

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohana 1:9).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Tabia njema ya Mariamu ilikuwa imeharibika. Alikuwa amechukia na kukasirika. Inawezekanaje rafiki zake anao waamini waseme uongo kama huo? Waalimu na hata watu wengine watafikiria ya kuwa alikuwa ameiba fedha za darasa. Aliendelea kuzitafuta katika kile chumba. Kumbe fedha zilikuwepo pale pale. Lazima ingekuwa hivyo. Kama hangezikuta zile fedha, basi kila mtu angemwona ya kuwa yeye ni mwizi.

Mara alisikia mtu akigonga mlangoni. "Naweza kuingia?" Martha aliuliza.

"Hapana!" Mariamu alimjibu kwa hasira.

Martha akamwambia "Nimefika kukuomba ili unisamehe."

"Mimi nilidhani ya kuwa wewe ni rafiki yangu, sasa kila mtu anadhani ya kuwa mimi ni mwizi kwa sababu yako!"

Je, kama wewe ndiye Mariamu, ungeonyesha roho ya upendo kwa Martha?



SURA YA KUMI

# MSALABA WA NAFSI YA KRISTO

Kusudi la Somo Hili: Nitajifunza kuishi kama Yesu.

Somo Kutoka: 1 Petro 2:19-25; Luka 14:33; Yohana 1:1-3

Vifungu vya Leo: 1 Petro 2:19-25; Yohana 1:1-3

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Basi, kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu" (Luka 14:33).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Yohana alibaki anamwangalia kaka yake aliyekuwa amekufa. Hangeweza kuzungumzana naye. Jambo hili lilimkumbusha wema wote wa kaka yake. Misaada ambayo alikuwa ameitoa kwa ile jamaa yake haiwezi kuelezeka.

Hata hivyo, Yohana hakumhesabu ndugu yake kama mtu aliyefanikiwa. Hakumaliza shule. Hakuwa na gari wala nyumba nzuri. Hakuwa na fedha katika banki.

Yohana alijiuliza, "Je, mtu anawezaje kuyahukumu maisha ya mtu mwingine? Aliangalia nyuso za kaka na dada zake wote waliokuwa wanalia na ambao walikuwa wamekaa karibu na lile kaburi wakiliangalia. Yusufu alikuwa na kazi ya uwakili, Daudi alikuwa mfanya biashara wa ule ukoo wote, Yakobo alikuwa daktari na yeye mwenyewe, Yohana, alikuwa waziri. Tena kila mmoja kati ya dada zake alikuwa ana kazi.

"Katika macho ya dunia sisi sote ni watu ambao wamefanikiwa sana katika maisha?" Alishangaa na kujiuliza,

Kazi ya Kristo pale msalabani imeelezwa katika Luka 19:10. Yesu alikuja kuokoa kile kilichopotea. Dhambi siyo kitu cha kukumbuka tena. Tunatubu dhambi zetu na kumwomba Mungu atusamehe. Yeye ametuahidi ya kuwa hatazikumbuka tena. Kama tutaomba msamaha tena kwa dhambi ile ile, Mungu atatuuliza, "Dhambi ipi?" Mungu husamehe na kusahau. Yesu alilipa deni. Maneno ya wimbo mmoja mashuhuri sana yanasema, "Deni yangu ya dhambi Yesu amelipa. Kwake msalabani, nilipewa uzima. Deni ya dhambi, msalabani, ilimalizikia, ni huru kabisa."

Kwa kuwa haikuwa lazima kwa Yesu kufa pale msalabani, kwa nini alifanya hivyo? Alichagua kifo kwa sababu aliwapenda wanadamu. Alikufa ili mwanadamu awe na mlango wazi wa kumfikia Mungu. Alikufa ili Roho Mtakatifu aje na kuwaongoza watu wake.

**Kazi ya Kufanya**

Yafikirie maswali yafuatayo kwa kuyatafakari au kwa kuandika majibu yake.

1. Je, mawazo ya Wayahudi yalikuwa yapi kutokana na kifo cha msalaba?
2. Ebu fikiria kuhusu maumivu aliyoyapata Yesu pale msalabani. Je, unafikiri mateso yake makubwa yalikuwa ni yale ya kimwili?
3. Je, unaweza ukafikiria jinsi itakavyokuwa kufa kwa ajili ya rafiki yako?
4. Je, utapenda kufa kwa ajili ya adui yako?
5. Haikumlazimu Yesu kufa msalabani, kwa nini alikufa?
6. Kifo cha Yesu pale msalabani kina maana gani kwako?





**Maelezo**

Ili tuweze kuufahamu mpango wa Mungu wa wokovu kwa mwanadamu, tunapaswa kufahamu ya kuwa Mungu ni Mungu mwenye upendo naye anao uwezo wa kusamehe wanadamu. Mtu anapotenda dhambi sana anakuta kila mara ya kuwa ni vigumu sana kuamini kuwa anaweza kusamehewa. Mara kwa mara mwanadamu anajaribu kuyahukumu matendo ya Mungu kutokana na jinsi mwenyewe alivyo. Jambo hili haliwezi kutendeka, yeye ni Mungu na mtu ni mwanadamu. Njia za Mungu zipo juu ya njia za mwanadamu.

Sura zilizopita katika kitabu hiki zimetuonyesha ya kuwa Mungu alifikia kikomo cha uvumilivu wake katika uhusiano wake na mwanadamu. Lakini licha ya machukizo yaliyofanywa na uasi wa mwanadamu alisikiliza kulia kwake katika kuomba msamaha. Je, Mungu anawezaje kuwa mwenye kusamehe kiasi hicho? Kwa hakika yeye ni Mungu wa msamaha na neema.

Msamaha ni jambo muhimu katika mpango wa Mungu kumletea mwanadamu wokovu. Katika 1 Yohana 1:3-5, Yohana anasema ya kuwa anatupa maelezo kuhusu yale aliyoyaona na kuyasikia kutoka kwa Bwana. Anawataka wale watakaosikia habari zake wasiwe na mawazo mengine kuhusu huo ukweli ambao anatuhakikishia.

Yohana alipata furaha inayotokana na utamu wa ushirika. Ametupa ushirika huo katika jina la Yesu Kristo.

Mungu ni nuru. Hakuna njia ambayo nuru hii ya Mungu katika Yesu inaweza kuzimwa. Yeye ni nuru ya kutuonyesha njia katika giza la dunia hii ya dhambi.

Yohana wa Kwanza 1:6-10 inawaeleza ndugu ya kuwa haiwezekani kushiriki pamoja na Bwana wakati ukiwa bado

unatembea katika giza. Giza ni maisha ya dhambi au ni kinyume cha uhai katika Kristo. Anatueleza kuhusu Nuru, yaani Yesu Kristo, na kusema ya kuwa twapaswa kuwa na ushirika wa sisi kwa sisi. Tunapokuwa na ushirika wa pamoja basi sisi sote twaweza kufurahi. Tutaufurahia ushirika huo kwa sababu tunaamini ya kuwa damu ya Kristo inao uwezo wa kututakasa sisi.

Hakuna mtu asiye na dhambi. Yohana ameeleza jambo hili upesi. Lakini Yohana, ambaye alipendwa sana na Yesu hakuachia hapo. Tunamwona Yohana akiwa na moyo wa kuzieneza habari njema za msamaha wa Mungu wa dhambi.

Uwezo wa kuweza kusamehe unatokana na Mungu. Msamaha haukuwa kitu rahisi kwa watu kukubali na kukielewa wakati wa Agano la Kale. Walifikiri ya kuwa kuomba msamaha ni kuonekana mnyonge. Historia inatuonyesha ya kuwa hata huko Israeli, msamaha haukuwa kitu kilichothaminiwa hata na wale wateule wa Mungu.

Hata hivyo katika Agano Jipya, Kristo ametuletea mawazo mapya ya msamaha. Alifundisha ya kuwa kusamehe ulikuwa wajibu wa kila mtu. Pia alifundisha ya kuwa tutoe msamaha kwa upesi.

**Mafunzo Ya Sura Hii Kwangu**

Kwa Kristo roho ambayo haikuwa tayari kusamehe ilikuwa ni dhambi isiyosameheka. Biblia inatueleza ya kuwa moyo usiosamehe ni dhambi ambayo Mungu hataisamehe. Soma Mathayo 18:34-35.

Lazima mambo fulani fulani yatekelezwe kabla ya msamaha kutolewa. Lazima pawepo na uhusiano kwa wale wanaosameheana. Lazima pawepo na nia ya kutubu kwa yule aliyeonea na yule aliyeonewa lazima awe tayari kusamehe. Yule mtoto mpotevu alipaswa kutubu kabla baba yake hajaweza kumsamehe.





Wakristo wanapaswa kufahamu ya kuwa kama Kristo hakufa msalabani, basi wokovu kwa mwanadamu haungepatikana. Kazi ya Yesu pale msalabani, pamoja na kifo chake vilifanya tukombolewe.

Kristo alifahamu ya kuwa ilikuwa lazima yeye kufa msalabani. Hii ndiyo njia pekee ambayo mwanadamu anaweza kusamehewa dhambi.

Katika Waebrania 10:9 Biblia inatueleza ya kuwa Yesu alikuja kufanya mapenzi ya Mungu. Kifungu cha 10 kinaeleza kuhusu kafara hiyo, yaani, mwili wa Yesu Kristo, ni kafara kwa wakati wote na yatosha kila kitu. Hiyo ndiyo kafara ya mwisho. Yenyewe imetimiza kati yake na haihitaji kufanywa tena.

"Imekwisha." Yohana alitumia maneno ya Yesu (Yohana 19:30). Yesu alitukomboa kwa upendo wake mwenyewe. Ukombozi wa mwanadamu ulitegemea tendo hili. Aliyarundisha maisha yake kwa Baba ambaye ndiye aliyempa.

Baada ya Yesu kufa, Biblia inatuambia ya kuwa alikaa mkono wa kuume wa Mungu, yaani Baba. Hapo ni mahali pa heshima. Ni ishara ya kuwa Yesu aliikamilisha kazi yake.

**Mafunzo Ya Sura Hii Kwangu**

Yesu alifundisha ya kuwa yeye, Mwana wa Adamu, lazima apate mateso. Wakati mmoja wanafunzi wake walianza kufahamu ya kwua kweli Yesu alikuwa Masihi, pia walijifunza kitu kimoja zaidi. Walijifunza kuwa Yesu alipoanza safari ya kuelekea Yerusalemu hakuwa anakwenda kuwa mfalme wa kidunia. Alikuwa anakwenda Yerusalemu kufa msalabani kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Jambo hili lilikuwa ngumu zaidi kwa wanafunzi wake kuelewa maana na lengo la Yesu. Tukumbuke daima ya kuwa, njia za Mungu zipo juu ya uwezo wa mwanadamu.

"Kwa nini alihatarisha maisha yake kwa ajili ya kijana asiye na thamani kama huyu?" Yusufu alilifikiria swali hilo kwa muda.

Kwa nini mtu anajitoa kulipa deni la mtu mwingine? Upendo peke yake ndilo jibu dhahiri. Yesu alikuwa na upendo mkubwa hata akawa tayari kutoa maisha yake kwa wenye dhambi wakatili.

**Maelezo**

Agano la Kale linatueleza habari za kuja kwa Masihi yaani, Yesu Kristo. Agano Jipya linaeleza kuhusu maisha ya Yesu, kazi zake, na njia ya wokovu kwa kupitia kwake.

Ebu tujaribu kuelewa kwa undani zaidi kuhusu msalaba kabla ya kufikiria kuhusu kifo cha Yesu pale msalabani. Kwanza, Wayahudi walichukia kitendo cha kumtundika mtu msalabani kama adhabu. Kwa Warumi tendo la kufa msalabani lilikuwa ni tendo ambalo waliliona kama la kudharauliwa sana. Tendo kama hilo waliona lifanyiwe watumwa.

Pili, tendo la kufa msalabani lilikuwa tendo la mateso mengi sana. Yule aliteseka sana hata ikiwa kama sehemu hiyo ni ya joto. Kuvimba kwa majeraha kuliwaletea maumivu mengi ya kichwa na kutetemeka.

Ingawa Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, alikuwa na mwili wa kibinadamu na alipata mateso kama sisi wenyewe tunavyopata. Alipata maumivu mengi sana pale msalabani, lakini maumivu mengi zaidi aliyoyapata ni kukataliwa na wale ambao alifika kuwaokoa. Yesu aliamua kufa kwa ajili ya dhambi za mwanadamu. Aliacha nyumba yake takatifu, na kuwa tayari kufa kwa ajili ya mwanadamu kwani anampenda.





Tunapaswa kufahamu ya kuwa Mungu hasamehi pasipo kutubu. Ili msamaha uweze kuwa wenye maana, basi huyu mtu na Mungu lazima warudie uhusiano ule wao waliokuwa nao kabla ya dhambi hiyo kutendeka. Jambo hili linahitaji matendo kwa upande wa Mungu na yule aliyekosa yaani mtu mwenyewe. Soma Kifungu cha Kukumbuka cha leo. Kinatueleza ni nini tunapaswa kufanya. Kwanza, ni lazima kutubu dhambi zetu. Pili, Mungu atatusamehe na tatu atatutakasa.

Kwa kuwa Mungu ni upendo, yuko tayari kusamehe dhambi. Ingawaje yeye ni Mungu wa upendo hatamsamehe mtu dhambi zake mpaka kweli amelijutia kosa hilo. Mungu ni Mungu wa haki, lakini vile vile ni Mungu mwenye kusamehe.

Basi katika hali kama hii furaha kamili itakuwepo. Mungu humrudisha mtu mpaka kwenye ile hali yake ya mwanzo, na msamaha wa Mungu unatokana na mawazo atakayokuwa nayo yule yule mtu aliyekosa.

Usidanganywe. Mungu hawezi kukubali dhambi. Kristo alikufa ili turudi katika uhusiano wa furaha na Mungu. Warumi 3:23-24 inatuambia, "kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu."

Upendo wa wokovu wa Mungu upo katika Yesu Kristo. Upendo wa aina hii huondoa dhambi kabisa na kwa hivyo unaondoa kizuizi kati ya Mungu na mwanadamu. Msamaha kwa njia ya huruma ya Mungu humrudisha mtu kwa Mungu.

**Kazi ya Kufanya**

Jadiliana na rafiki au andika majibu ya maswali yafuatayo:

1. Je, umeshawahi kumsamehe mtu kwa kosa alilokufanyia? Je, baada ya kumsamehe alijisikia namna gani?

2. Je, ni mara ngapi Mkristo anapaswa awe tayari kusamehe mtu mwingine? (Soma Mathayo 18:21-35.)

3. Tunapaswa tufanye nini kabla Mungu hajatusamehe? Je, umefanya kitendo hicho?

4. Je, tunaweza kumpenda Mungu na kumchukia (kukataa kumsamehe) ndugu yetu? Soma 1 Yohana 4:20.

5. Je, kuna mtu ye yote aliyekuchukiza leo? Je, unaweza kumsamehe?



SURA YA TISA

# MSALABA NA UKOMBOZI

Kusudi la Somo Hili: Nitajifunza kuwa Yesu alilipa deni langu la dhambi.

Somo Kutoka: Luka 19:10; Mathayo 1:21; Waebrania 10:8-18

Vifungu vya Leo: Waebrania 10:8-18

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao" (Mathayo 1:21).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Kila mmoja katika darasa alikuwa akiongea kuhusu tendo la kishujaa lililotendeka. Yakobo alisikia hangaiko alipofungua mlango.

Yusufu alimwuliza, "Je, umesikia habari za Marko?"

Yakobo akamjibu, "Hapana, ni kitu gani kimetokea?"

"Walipata ajali. Yeye yuko hospitalini na madaktari wanasema ya kuwa hataweza kutembea tena."

Yusufu aliendelea kueleza habari za ushujaa wa Marko. Baadhi ya vijana katika kijiji walikuwa wakipigania mpira. Kijana mmoja ambaye mara kwa mara alifanya hila mbaya kwa wengine alichukua mpiga na akakimbia barabarani. Marko aliona gari linakuja na akamsukuma yule kijana kutoka barabarani, lakini Marko alianguka katikati ya barabara. Lile gari lilimkanyanga miguu yake na kuivunjavunja.

1. Je, neno "wokovu" lina maana gani kwako?

2. Je, kuna nini katika wokovu? (Kumbuka hatua zile tatu ulizojifunza katika somo la 5.)

3. Mungu amechagua mwanadamu kwa kazi gani nyingine zaidi ya wokovu?

4. Kama Mungu anapenda kila mtu aokolewe, kwa nini wengine wanapotea?

5. Orodhesha vipaji vile ulivyonavyo. Fikiria jinsi kila kimoja kitakavyotumika katika utumishi wa Mungu (hata kama ni kuchota maji).

6. Soma Zaburi ya 139. Je, unaamini ya kuwa Mungu anafahamu mambo yako yote? Je, Mungu anao mpango kwa ajili ya maisha yako? Je, unafahamu mpango huo?



SURA YA TANO

# MUNGU ALITUAHIDI MASIHI

**Kusudi la Somo Hili: Nitajifunza kuwa Yesu anaweza kuyabadilisha maisha yangu.**

**Somo Kutoka: Isaya 9:27; 53:2-6; Yeremia 33:13-16; Mika 5:2**

**Vifungu vya Leo: Yeremia 33:12-16; Isaya 9:6-7**

**Kifungu cha Kukumbuka**

> **"Maana, kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani" (Isaya 9:6).**

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

**Hapo zamani za kale miungu ya ndege ilikuwa ikijadiliana kuhusu tatizo fulani. Walitaka kutoa ujumbe maalum kwa ndege wote duniani. Ndege wote walitakiwa wabadilishe jinsi wanavyoishi au sivyo wote wangekufa.**

**Ndege mmoja akashauri, "Labda tutaweza kuyaandika maneno hayo katika mawingu. Mmoja wetu anaweza kuruka juu sana na kuyaandika maneno hayo ili wote waweze kuyaona."**

**Mwingine akasema, "Jambo hili halitawezekana. Hawataweza kuyasoma."**

**Mwingine alipiga kelele na kusema, "Mimi naelewa. Tutampeleka malaika apeleke huo ujumbe kwa mmoja wao naye atawaambia wengine."**

"Hawataamini ujumbe huo."

Kiongozi wao akasema, "Kuna njia moja tu. Mmoja wetu lazima awe ndege. Naye ataishi pamoja nao. Nao wataweza kuona ni aina gani ya maisha yenye mfano mzuri wanaopaswa kuishi. Kwa hakika wataweza kuamini na hawatakufa. Tutaweza kuwapelekea ujumbe wetu kwa kushirikiana pamoja nao."

**Maelezo**

Mungu katika huruma yake aliangalia mbali zaidi ya hali ya dhambi ya mwanadamu. Kama Mungu alikuwa atekeleze mpango wake wa kumwokoa mwanadamu, lazima pia angeangalia mbali zaidi ya ile ghadhabu yake.

Mungu alikuwa amechukizwa na dhambi za mwanadamu. Kwa njia ya manabii wote Mungu ameeleza kuhusu kuja kwa Masihi ambaye atamwokoa mwanadamu kutoka dhambini. Atalipa deni kubwa. Mungu atampeleka Mwana wake. Ataona atakavyopata mateso na kufa kikatili pale msalabani. Mungu anatutegemea kuwa tayari kulipa deni kama hilo. Hiyo ndiyo njia yake ya kutupa ujumbe wake.

Katika Yeremia 33:14-16, tunasoma kwa kifupi kuhusu unabii wa Mungu juu ya Masihi yule atakayekuja. Aliahidi nyumba ya Israeli kuwa mbegu ya Israeli haitakuwa na mwisho. Wayahudi walikuwa ni taifa ambalo lilikuwa na mawazo mengi sana kuhusu mambo ya baadae. Walimtegemea sana yule atakayekuja na ambaye atawaletea haki na kutoa hukumu. Wayahudi walitegemea ya kuwa mtawala wa Israeli atakuwa mwenye nguvu nyingi. Tena walifikiri kuwa Masihi atakuwa kiongozi ambaye atawaokoa kutokana na maadui zao. Wao hawakujua hata kidogo kuwa kiongozi huyu atakuwa wa kimungu.





msamaha. Mungu humtafuta mwenye dhambi. Mwanadamu humtafuta Mungu kwa sababu Mungu ndiye aliyemtafuta kwanza.

Uamuzi wa Mungu wa kuokoa haukuwa wa ghafula tu. Huu ndio uliokuwa mpango wake kutoka mwanzo. Mpango wa wokovu ulikuwa kusudi la Mungu tangu kabla ya kuwepo kwa msingi wa dunia. Mungu hakuchagua baadhi ya watu waokolewe na wengine kuangamia. Anataka watu wote waokolewe. Kutenda dhambi kwa makusudi ndicho kitu kinachomfanya mtu asiokolewe. Mungu amefanya anayopaswa, bali yeye amempa mwanadamu uamuzi wa kuamua mambo yake yeye mwenyewe.

Mungu hachagui mtu kwa wokovu tu bali pia kwa kazi ya utumishi. Mungu anapenda kufanya mema kwa njia ya mwanadamu. Tena hii sio kazi tu ya wachungaji na wamisheni. Ni kwa wale wote wanaomwamini Yesu Kristo. Hakuna mtu hata mmoja awezaye kusema ya kuwa yeye ni mzee sana au mdogo sana kwa kazi ya utumishi. Kristo alikuja ili alete wokovu kwa kila mmoja. Kwa njia hiyo, Kristo amemwita katika utumishi kila mtu, pasipo kujali uwezo wake alionao.

Kusudi la Mungu na mpango wake kwa maisha yako linahusiana na tendo la wokovu. Mwandishi wa Zaburi anatueleza ya kuwa kabla ya kuzaliwa kwetu, kila siku ya uhai wetu ilikuwa imeandikwa katika kitabu cha Mungu (Zaburi 139:16). Je, unataka kuutafuta mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha yako? Yesu ameahidi ya kuwa atakufungulia mlango kama ukimwomba. Huu ndio wakati wa kufanya uamuzi huo. Usichelewe.

**Kazi ya Kufanya**

Yafikirie maswali haya na kuyajadili au kuandika majibu yake.

Soma Yohana 6:44-51. Mtu anapookolewa anakuwa ameokolewa sio kwa bahati au ajali. Anakuwa ameokolewa kwa sababu huo ni mpango wa Mungu. Mungu anamwokoa mtu kwa sababu anapenda kufanya hivyo. Anamwokoa mtu fulani, kwa wakati maalumu na katika hali fulani kwa sababu anapenda kufanya hivyo. Kazi ya mwanadamu ni kumruhusu Mungu ayaokoe maisha yake kwa njia ya kumkubali Mwana wa Mungu, kama Mwokozi wake. Maandiko ya kifungu cha 44 yanasema, "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka...." Yesu anasema Mungu humpeleka mtu kwa Kristo. Kristo hutoa kwa kila mmoja uzima wa milele.

**Mafunzo Ya Sura Hii Kwangu**

"Je, wokovu ni nini?" Hili ndilo swali kubwa. Wakati mkosaji anapotubu kweli dhambi zake na kumwamini Kristo, anakuwa amefanya hivyo kwa sababu Mungu ndiye aliyetenda jambo hilo ndani yake. Mwanadamu hawezi kumwendea Mungu kwa nguvu zake yeye mwenyewe.

Jambo hili halipo katika asili ya mwanadamu. Ni lazima awe amesukumwa na Mungu. Mtu akiziacha dhambi ni kwa sababu Mungu huwavuta wanadamu kwake. Jambo hili linaitwa "kuhukumiwa na dhambi."

Hapo ndipo watu wa Mungu wanapoonekana walivyo. Mungu hutenda kazi kupitia kwa watu. Anawatumia watu wake ili waweze kuwafundisha wengine. Anatumia injili yake na mashirika mengine mbali mbali ambayo yanahusika katika kuendeleza injili. Huingia katika mioyo yetu na dhamira zetu. Hatujui Mungu anatenda kazi kati ya nani. Ila kila mara tunapaswa kuwa macho ili tuwasaidie wengine waelewe ya kuwa Mungu anataka kuwaokoa nao pia.

Mungu hufanya kazi ndani yetu tena hutufanya tutubu na kuwa na imani. Hufanya kazi ndani yetu ili tuweze kuomba





Nabii Isaya katika Isaya 9:6-7 ameeleza kusudi la huyu Masihi atakayekuja kama Mungu alivyotaka jambo hilo lifahamike. Wao Wayahudi walimfikiria huyo Masihi kuwa ni mtawala wa duniani. Isaya ameeleza kuhusu ufalme wa Daudi, naye Yesu alizaliwa katika ukoo wa Daudi. Wito wa Kristo ulikuwa ni wito wa mambo yaliyo juu ambayo ni zaidi ya kuwa mfalme wa hapa duniani.

Hakuna mtu wa vivi hivi ambaye angeweza kuzaliwa na akaitwa Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Lazima jambo la kimungu lilihusika. Katika kitabu cha Danieli mtawala huyu ajaye ameonyeshwa kama mtu katika umbo la kibinadamu mwenye tabia ya Kimungu.

Kwa njia ya mtu huyu wa Kimungu, Mungu ataanzisha ufame wake hapa duniani. Wazo lao lilikuwa ni lile lile la mwana wa Kifalme ambaye ataleta ushindi na mafanikio kwa taifa la Israeli. Kutokana na imani yao ataweka ufalme wake huko Yerusalemu. Hii ndiyo sababu watu wengi kiasi hicho walikuwa tayari kumpokea Yesu alipoingia Yerusalemu. Mawazo ya kiroho yalitakiwa kumtambua Yesu kama Mwokozi aliyeahidiwa ambaye ataliokoa taifa hilo kutoka katika dhambi zake. Ni wale tu ambao walikuwa na mawazo ya kiroho ndio waliotambua ya kuwa Yesu alikuja kuokoa.

Yesu anayeelezwa katika Mika 5:2 siye ambaye Wayahudi walimtaka. Wao walitaka mtu ambaye angechukua hatua mara moja. Pia walitegemea zaidi kupinduliwa kwa utawala wa Kirumi kuliko mambo mengine ya Kiroho.

**Mafunzo Ya Sura Hii Kwangu**

Mungu alifahamu ya kuwa mwanadamu ametenda dhambi kwa hivyo mwanadamu alitengwa na Mungu. Mwanadamu alimhitaji Mkombozi. Mungu aliahidi

kumpeleka Mwanawe awe ndiye huyu Mkombozi. Kwa kuwa alikuwa hana dhambi, ni Yesu Kristo peke yake ambaye angeweza kulipa deni la dhambi ya mwanadamu.

Soma Isaya 53:2-6. Vifungu hivi vinatupa picha halisi ya Kristo hapa duniani. Alidharauliwa na kukataliwa. Alichukua uzito wa dhambi za dunia. Aliteswa na kufa ili kila mtu aweze kupata uzima wa milele.

Labda bado umechagua kufuata njia yako mwenyewe kama ilivyoelezwa katika Isaya 53. Kama kondoo unaweza ukapotoka haraka. Huu ndio wakati wa kuyachunguza maisha yako. Je, unaitafuta njia iliyo nzuri? Je, umetosheka jinsi ulivyo? Je, unajaribu kuishi maisha ya Kimungu au unaweza ukashawishika katika kutenda dhambi?

Ahadi ya Mungu ilikamilika wakati alipompeleka Mwanawe wa pekee duniani. Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, alikuja kutokana na mpango wa Mungu wa wokovu wa wanadamu kutoka katika nguvu za Shetani.

Ni kwa njia ya kujitambua kiroho tu ndipo mwanadamu anaweza kumpokea Mwana wa Mungu. Kila jengo la kanisa, kila picha ya msalaba ni ukumbusho kwetu wa yale Mungu, katika upendo wake aliyomtendea mwanadamu mwenye dhambi. Yesu anagonga mlangoni mwa moyo wako. Ni kwa njia tu ya mtu mmoja mmoja kukutana na Kristo ndipo ataweza kutambua ahadi za Mungu kuhusu Masihi. Ukitaka kukutana naye ni lazima uache dhambi na kumfuata yeye. Njia ipo wazi. "...Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka..." (Matendo 16:31).

Mungu alituahidi Masihi. Alimtoa Mwanawe wa pekee. Kila mara Mungu hutimiza ahadi zake. Yesu anaweza kubadilisha maisha yako. Ni wajibu wako kumkubali au kumkataa Mwana wa Mungu.





kuwa walikuwa na mtoto mchanga, iliwabidi kuteka maji kila siku. Mwanamke huyu alisaidia kila siku kuchota maji.

"Ni afadhali kuona hotuba kuliko kuelezwa kuhusu ibada," maneno hayo yalimjia Miriamu. Alifahamu ya kuwa alikuwa ameshuhudia hotuba ya upendo.

**Maelezo**

Maandiko yanatufundisha ya kuwa sio tu kuwa Mungu anao mpango maalumu wa kukamilisha katika historia ya mwanadamu, bali anao mpango maalumu kwa kila mtu. Mungu alituchagua kwa ajili ya kazi ya wokovu na utumishi.

Wokovu katika Agano la Kale ni tofauti na wokovu katika Agano Jipya ambao upo katika Yesu Kristo. Watu wa Agano la Kale walizishika sana sheria, pasipo shaka yo yote. Agano lilikuwa ni kati ya Mungu na taifa la Israeli. Watu hao waliitwa "taifa teule la Mungu" naye alifanya ahadi nyingi nao.

Mungu alimwahidi Abramu, Baba wa taifa la Israeli ya kuwa kizazi chake kitakuwa cha watu wengi na kuwa atawabariki. Yeye alitimiza kila ahadi aliyowaahidi bali wao wana wa Israeli hawakupokea ahadi hiyo maalum ya Mungu. Hawakumpokea Mwana wa Mungu kama Masihi. Bado hata leo wanangoja kuja kwa Masihi.

Yesu alipokuja alifanya kazi yake kwa mtu mmoja mmoja. Alituletea mpango wa Mungu wa wokovu kwa ye yote atakayemwamini.

Utumishi wa Yesu ulikuwa ni pamoja na kuwa kati ya watu. Utumishi wake ulikuwa wa mtu mmoja mmoja na ni hivyo hadi leo. Alitoa msamaha, akaponya na akawaita watu wafanye kazi ya utumishi. Hata leo watu wakimwamini Yesu, watakuwa sehemu ya wateule wa Mungu.

SURA YA NANE

# MPANGO WA MUNGU WAHUSU WOKOVU

Kusudi la Somo Hili: Nitajifunza kuhusu mpango maalumu wa Mungu wa utumishi kwangu.

Somo Kutoka: Luka 19:10; Yohana 6:44-51; 1 Yohana 4:9

Vifungu vya Leo: Yohana 6:44-51; 1 Yohana 4:9

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Mimi ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka mbinguni; mtu akila chakula hiki, ataishi milele. Na chakula nitakachotoa mimi ni mwili wangu..." (Yohana 6:51).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Kuchota maji ni sehemu ya maisha. Shughuli hiyo ni ya kila siku; haina mwisho. Kazi hii inaweza kuwa ngumu zaidi kama mnaishi mlimani na maji yenyewe yako umbali wa maili kama mbili hivi. Hivi ndivyo ilivyokuwa siku hiyo.

Miriamu alianza kuupanda mlima huku akiwa amelemewa na maji mazito aliyokuwa ameyabeba. Akitoka shuleni ataendelea na shughuli hiyo hiyo. Mbele yake kulikuwepo na wanawake wawili. Ruthu alimsalimu. Mazungumzo yao yaliendelea walivyoendelea kupanda ule mlima. Baada ya kutembea kiasi, mwanamke mmoja alisimama karibu na nyumba fulani. Alinyosha mkono na kuwasalimu ndipo Ruthu alipoeleza kuhusu huyu rafiki yake. Yule mwenzake hakuwa amefika nyumbani kwake bali kwa jirani yake. Kwa





**Kazi ya Kufanya**

Jibu maswali yafuatayo:

1. Kwa nini Mungu aliona ya kuwa ilikuwa ni lazima kumpeleka Masihi duniani?
2. Je, Wayahudi walimngojea Masihi wa aina gani?
3. Kwa nini Yesu alikataliwa kama Masihi?
4. Je, Isaya alikuwa na maana gani aliposema ya kuwa kama kondoo tumepotea? Fikiria njia mbali mbali ambazo zimekufanya ukafanya mambo yaliyokuwa maovu.
5. Utawezaje kufahamu pasipokuwa na wasiwasi ya kuwa Yesu ni Masihi wa kweli?
6. Je, unaweza ukataja wakati wo wote ambao Yesu hakutimiza ahadi zake?
7. Je, leo utamruhusu Yesu ayabadilishe maisha yako?

SURA YA SITA

# MPANGO WA MUNGU WA UKOMBOZI

Kusudi la Somo Hili: Nitajifunza kusudi la Yesu kwangu mimi ninayepaswa kukombolewa.

Somo Kutoka: Waefeso 1 na 2

Vifungu vya Leo: Waefeso 1:2-12

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake" (Waefeso 1:7-8).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Yohana alikuwa amemaliza mwaka wake wa kwanza katika chuo kikuu. Mwaka ule ulibadilisha maisha yake. Huko alikutana na Sara, msichana mzuri wa Kikristo, aliyekuwa amemweleza jinsi ya kuwa Mkristo.

Akiwa na furaha ya wokovu wake moyoni, Yohana hakuweza kungoja mpaka afike nyumbani. Babu yake alikuwa ameuza mbuzi wake wengi ili amlipie ada yake shule. Alifurahi sana Yohana alipopata alama za juu katika mtihani hata kuweza kuingia chuo kikuu. Kwa sasa Yohana alipenda kushiriki pamoja na babu yake kuhusu uamuzi muhimu alioufanya kwa ajili ya maisha mwake.

Msichana mmoja wa kijijini kwake alimwongoza kuelekea katika msitu fulani. Yule babu alisimama peke yake chini ya mti fulani wa kutambikia. Pale karibu Yohana aliweza kunusa harufu ya kondoo wa kuteketezwa aliyekuwa akichomwa juu ya moto.





**Kazi ya Kufanya**

Fikiria mambo yafuatayo:

1. Je, Yesu anahusianaje na historia ya Biblia?
2. Je, historia ya Biblia imetuonyeshaje upendo wa Mungu?
3. Je, maisha yako yanawezaje kuwa mfano kwa watu wengine jinsi watakavyoabudu na kumtumikia Mungu?
4. Je, wewe ni mfano huo?

unatupa maana mpya katika Agano Jipya katika njia ya Yesu Kristo.

Kule hekaluni tumemwona mzee Simoni akimsalimu mtoto Yesu ambaye ataleta wokovu duniani. Maandiko yanatueleza ya kuwa hata Maria na Yusufu walishangazwa na maneno ya Simoni. Biblia inatuambia ya kuwa Simoni alikuwa amejawa na Roho Mtakatifu. Soma habari hizo katika Luka 2:25-32.

Manabii walieleza kuhusu kuja kwa Mwokozi. Jambo hili lilithibitishwa katika historia. Yesu alitimiza ahadi hizi katika Isaya 53: kuja kwake ni kama mzizi katika nchi kavu; alidharauliwa na kukataliwa na watu, mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko. Miaka mingi kabla ya kuzaliwa Yesu, mtu huyu wa Mungu alieleza kuhusu mpango wa Mungu wa wokovu kwa njia ya Mwanawe pekee. Yesu angezichukua dhambi za ulimwengu kwa watu wote wa nyakati zote. Wala hangefungua kinywa chake kujitetea mbele ya wadai wake. Jifunze kuhusu utumishi wa manabii katika kitabu cha Matendo. Soma jinsi injili inavyowahusu hata wale ambao si Wayahudi. Hata Watu wa Mataifa walizisikia habari za injili kuhusu Yesu (Matendo 13:48). Baada ya Petro kuona maono kutoka kwa Mungu, alikwenda kuonana na Kornelio. Mahubiri yake yameandikwa katika Matendo 10:34-43. Waamini wa Kiyahudi walishangazwa na Watu wa Mataifa. Kwani nao pia waliamini na kubatizwa.

Ni jambo ambalo ni wazi katika Biblia nzima ya kuwa Mungu ni Mungu anayemjali mtu mmoja mmoja. Agano Jipya na Agano la Kale ni historia ya ushuhuda wa upendo wa Mungu na kusudi lake katika dunia. Kwa kusoma maandiko haya kwa makini Wakristo wataelewa ya kuwa Mungu anampenda mtu mmoja. Mungu anampenda kila mtu mmoja, mmoja kama vile alivyomtuma Mwanawe kuteswa na kufa kwa ajili ya wanadamu wote.





Yohana alifikiria, "Je, bado anamtafuta Mungu kwa njia ya kutambika?" Yohana alijisemea, "Mungu, nisaidie ili niwe na maneno mazuri ya kueleza kuhusu Mwanao Yesu." Hiyo ndiyo iliyokuwa sala yake alipoamua kumwendea babu yake.

**Maelezo**

Masihi alikuja na kuchukua mzigo wa dhambi za wanadamu. Kama Masihi hangekuja, basi wanadamu wa leo hii hawangekuwa na uhusiano na Mungu. Hii maana yake ni kuwa mwanadamu angekuwa bado anafanya kafara madhebahuni. Sio hilo tu, bali pia hata kama mtu atakuwa mfuasi wa Yehova, basi angetakiwa azifanye kafara za hekaluni.

Yesu alibadilisha mambo hayo yote. Kwa sababu ya Yesu Kristo, Wakristo mmoja mmoja wanaweza kumwendea Mungu wakati wo wote wanaopenda. Hawapo tena chini ya mila za kufanya kafara. Kitu ambacho ni muhimu ni uhusiano wa mtu alionao na mwana wa Mungu, Yesu.

Mambo haya hayakutokea ghafula tu. Ni mpango ambao Mungu aliupanga kwa makini. Tumaini la watu wengi leo lipo katika wema wa Mungu, ambaye mwanadamu amemkosea. Tumaini hili ndilo linalomfanya mwanadamu aweze kuelewa mpango wa Mungu wa wokovu.

Paulo katika barua yake kwa Waefeso anawasalimu na kumsifu Mungu. Soma Waefeso 1:2-6. Ndipo mtume huyu anapotueleza kiini hasa cha jambo lenyewe. Anasema ya kuwa Mungu alituchagua kabla ya kuumbwa kwa dunia. Ni jambo ambalo ni dhahiri kuona ya kuwa Mungu hakuota ndoto tu kuhusu jambo fulani wala hakufikiria tu jinsi ya kuondoa dhambi kutoka katika maisha ya mwanadamu.

Mungu ni mwenye kufahamu yote. Kutoka mwanzo wa dhambi kusudi lake lilikuwa ni moja tu. Kumpeleka Kristo

afe ili wale wanaomwamini waweze kuwa na uzima wa milele. Soma Waefeso 1:7-12. Mungu alifahamu ya kuwa Yesu atalipa deni la uasi wa mwanadamu. Kwa njia ya Yesu vitu vyote mbinguni na duniani vimeunganishwa pamoja. Pia kwa njia yake mwanadamu amepewa ufunuo wa mpango wa Mungu wa wokovu.

Kudhani kuwa watu wote wanakataa upendo wa Mungu kwa ajili ya laana ya dhambi ni jambo linalotisha sana, ila hapo sio mwisho. Kuokoka kwa mwanadamu kunatokana na kutokata tamaa ambayo ni picha ya tabia ya Mungu. Mungu ni Baba wa upendo mtakatifu.

**Mafunzo Ya Sura Hii Kwangu**

Ni jambo lililo muhimu kutambua ya kuwa Mungu ana kusudi na maisha ya kila mtu. Yaani Mungu ni Baba wa wote. Akiwa kama Baba analo kusudi linalohusiana na uumbaji wake.

Uumbaji unawahusu watu wote mahali po pote walipo. Hakuna tofauti ikiwa watu hao wanaishi kijijini au mjini. Pia kwake si kitu kama wanafanya kazi katika viwanda, ofisini au ni wachungaji wa ng'ombe na mbuzi. Wala, taifa, wakati au kabila lao kwake si kitu, Mungu anao mpango kwa kila mmoja.

Kusudi la Mungu ni kurudisha uhusiano mkamilifu alioutaka alipoumba mwanadamu. Soma Waefeso 2:4-6. Hilo ndilo lililokuwa kusudi lake la kumwumba mwanadamu. Yesu ndiye hiyo njia ya kumrudisha mwanadamu kwake. Dhambi ilileta kutengana. Njia iliyopo tu ya kuondoa ufa huo kati ya Mungu na mwanadamu ni Yesu Kristo.

Je, Mkristo mwenye shukrani anawezaje kuwaonyesha watu wengine upendo wa Mungu? Katika Waefeso 2:10





Soma kuhusu ahadi za Mungu katika Mwanzo 9:9-17. Kabla ya maandiko haya kuna maelezo kuhusu gharika. Mungu aliamua kuiangamiza dunia kwa maji. Waliookolewa ni Nuhu, jamaa yake na wanyama wale tu ambao aliwaweka katika safina.

Ingawaje gharika ilileta maafa mengi bado kulikuwepo na matumaini. Mungu alifanya maangano na Nuhu. Pia kutakuwepo na upinde wa mvua katika mawingu kila wakati. Hata baada ya majaribu na kuangamia, Mungu anapatikana kama mwanadamu atamtambua yeye.

Historia ya Agano la Kale ni wito wa Mungu kwa Abramu ambao ulileta kusudi jipya kwa Mungu na uumbaji wake. Kwa sababu ya imani ya Abramu, Mungu alichagua kufanya agano naye. Soma Mwanzo 12:1.

Hata jamaa yake Abramu walikuwa ni watu maalumu kwa ajili ya kusudi kubwa la Mungu kwa dunia. Mungu hakumaanisha ya kuwa mataifa mengine hayatahusishwa. Maana yake ni kuwa mataifa mengine yatamwiga Abramu pamoja na kizazi chake jinsi ya kuabudu.

Hivi ndivyo inavyotakiwa hata leo katika jamii ya Kikristo. Ushirika wa Wakristo unapaswa kuwa mfano wa yale yanayompendeza Mungu.

Katika kitabu cha Kutoka tumesoma jinsi Mungu alivyomwongoza Musa pamoja na wana wa Israeli kutoka utumwani huko Misri. Wayahudi walikuwa utumwani. Farao hakuwaruhusu wawe huru kwa sababu walikuwa watumwa wake. Mungu alikuwa na mpango wake nayo mapenzi yake yalitimia. Kutoka 15 ni wimbo wa kumsifu Mungu kwa kuwaokoa watu wake.

**Mafunzo Ya Sura Hii Kwangu**

Je, historia ya Biblia ina maana gani kwangu? Je, inahusiana na maisha yangu leo? Mpango wa Mungu

Yakobo akiwa katika wakati uliopo aliweza kusikia masikioni mwake jinsi profesa wa historia anavyomweleza historia ambayo ilikuwa inaingia masikioni mwake. "Kujifunza historia kunaweza kuwa ni kitu kizuri sana kama watu hawatafikiria tu kuhusu mitihani wanapozungumzia historia. Mara kwa mara wanajifunza tu kwa ajili ya kupita mtihani halafu baadae wanasahau yale yote waliyojifunza.

"Tunaweza kujifunza mambo mengi kutokana na historia. Katika sehemu zile ambazo historia haijaandikwa vitabuni, watu mbali mbali wa kabila hilo wameeleza habari za historia yao mara nyingi. Hadithi hizi zinaelezwa kutoka kizazi kimoja hata kingine. Jambo hili ni muhimu sana kwa kila kabila. Kila kabila lina historia yake na linapaswa kujivunia. Linapaswa kukumbuka historia yake ili liweze kuhifadhi utamaduni wake."

Yakobo alifurahi alipoyasikia yale yote kuhusu historia yao ya kale ikisimuliwa katika wakati uliopo.

**Maelezo**

Hata Wakristo nao wanaweza kuielewa historia yao pia. Mungu amelipanga jambo hilo hivyo. Biblia inatupa historia ya wateule wa Mungu, hata Wakristo wa leo. Katika wakati wote wa historia Mungu amempa mwanadamu kiu kubwa ya kumtafuta na haja kubwa ya kumfahamu. Mwanadamu hana mapumziko mpaka atakapopumzika katika Mungu. Historia ya dini ni rekodi ya mwanadamu katika kumtafuta Mungu. Hata hivyo kumtafuta huko hakujawa bure kwa sababu ya upendo na huruma za Mungu.

Hata mwanadamu alipotenda dhambi, Mungu alimpa Hawa tumaini. Soma Mwanzo 3:15. Mwanamke huyu wa kwanza aliweza kuzaa watoto. Tena kizazi hicho kitaendelea.





tunasoma ya kuwa, Mungu alipanga kuwa Yesu ndiye atakayempa mwanadamu maisha mapya. Mpango wa Mungu ulikuwa kwamba maisha yatumiwe katika kuwasaidia wengine. "...sisi tuliotangulia kumwekea Kristo tumaini letu" (Waefeso 1:12).

Mtu mzee anapokuwa na mahitaji, roho wa Kristo aliye ndani ya maisha ya mwamini atamfanya kumsaidia hata kama si ndugu yake. Watu wana njaa, wako pweke, wako katika hali ya wasiwasi, wengine ni wagonjwa na wengine wako gerezani. Mathayo 25 inatufundisha baadhi ya mahitaji yao. Ni jambo la kujihoji kwa Mkristo mtumishi wa kanisa (au yule ambaye si mtumishi) kwa wale wenye mahitaji.

Tunaweza kutenda mambo mazuri badala ya mambo mabaya kwa sababu roho wa Kristo huwasaidia wafuasi wake. Roho wa Yesu hutusaidia ili tuweze kuwasaidia wengine. Upendo wa jinsi hii utawavuta wengine kwa Yesu Kristo.

Kumbuka ya kuwa Kristo hakujali aina fulani ya watu tu. Alikuja kwa ajili ya wote. Huu ndio msingi wa ushuhuda wa Kikristo.

**Kazi ya Kufanya**

Fikiria mambo yafuatayo:

1. Je, uhusiano wa mtu na Mungu ulikuwaje kabla ya Kristo kuja duniani?

2. Kristo ni Mwokozi wa kila mtu. Orodhesha njia ambazo Mkristo anaonyesha ya kuwa anaishi kama Kristo kwa wale waliomzunguka.

3. Je, kuna maana gani mtu anapokuwa na uhusiano na Yesu Kristo?

4. Je, wewe unao uhusiano huu na Yesu Kristo?

5. Kariri zile hatua 3 za wokovu ambazo mwalimu wako alifundisha katika somo la 5 ikiwa bado hujafanya jambo hili. Mweleze ushuhuda wako na rafiki.



SURA YA SABA

# MPANGO WA MUNGU UPO KATIKA HISTORIA

Kusudi la Somo Hili: Nitajifunza jinsi ya kuhusisha historia ya Biblia na maisha yangu.

Somo Kutoka: Mwanzo 9:9-17; 12:1; Kutoka 15; Luka 2:25-32; Isaya 53

Vifungu vya Leo: Mwanzo 3:16; 9:9-17; 12:1-2

**Kifungu cha Kukumbuka**

> "Na agano langu nitalithibitisha nanyi; wala kila chenye mwili hakitafutwa tena kwa maji ya gharika; wala hakutakuwa tena gharika, baada ya hayo, kuiharibu nchi" (Mwanzo 9:11).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Yakobo alikuwa karibu kumaliza safari yake. Njia ya kichochoro inayoelekea nyumbani kwake ilikuwa mbele yake. Baada ya kuona ya kuwa likizo sasa imekaribia na kuwa ataziacha kazi za shule, alipumua kwa nguvu. Mawazo ya kwenda nyumbani, hali yenyewe ilivyokuwa hata na harufu na sauti mbalimbali zilimfurahisha. Alipokuwa akiupita mti mmoja ambao aliuzoea sana tangu utotoni alikumbuka enzi za utoto wake. Mawazo yake yalimpeleka kwa yule mzee kikongwe. Wakati huo watoto wengi walipenda kukimbia na kupita mbele yake ili waweze kupata mahali pazuri pa kukaa chini ya mti. Mzee alikaa juu ya kibao kidogo cha kukalia na watoto walikaa kumzunguka.

Alianza hadithi yake kwa kuwaambia, "Ilikuwa ni zamani sana hata kabla ya mimi kuzaliwa."